Nipashe
Jumanne Novemba 3, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0580388
www.ippmedia.com
The Guardian digital
nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710




UKURASA 11

**ADAIWA** kuua mke, shemeji kwa shoka

UKURASA 4



**CCM** yatangaza nafasi uspika, naibu, mameya

UKURASA 4

# Dk. Mwinyi kuunda serikali ya maridhiano

UKURASA 2



Jaji Mkuu wa Zanzibar, Omar Othman Makungu, akimwapisha Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi (kulia), kuongoza Zanzibar katika uwanja wa Amaan, Zanzibar jana. **PICHA: IKULU . Picha zaidi Uk. 8.**

# Vigogo wa CHADEMA mbaroni tuhuma ugaidi

UKURASA 2

## YALIYOMO

**UKURASA WA 3**

**MAANDALIZI KIAPO CHA JPM YAPAMBA MOTO**
SERIKALI imeendelea kuandaa mazingira ya kuapishwa kwa Rais mteule Dk. John Magufuli, ambaye ataapishwa Alhamisi...

**UKURASA WA 4**

**MAJENGO YA SERIKALI YACHOMWA, MAGARI YAHARIBIWA KISA UCHAGUZI**
BAADHI ya wananchi wenye hasira mkoani Lindi, wanadaiwa...

**UKURASA WA 5**

**ANAYETUHUMIWA KUPORA SANDUKU LA KURA ASAKWA**
MKUU wa Wilaya ya Lindi, Shaibu...

**Profesa Lipumba ataja sababu CUF kutoshiriki tena uchaguzi mkuu**

UKURASA 3

**MICHEZO** **MO, HANS POPPE SASA WALIA HUJUMA SIMBA** UK. 24

**MAONI,**

# Dk. Mwinyi kuunda serikali ya maridhiano

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

RAIS mpya wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema ataunda serikali itakayoenzi maridhiano ya kitaifa kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar.

Akihutubia kwa mara ya kwanza baada ya kuapishwa kuwa Rais wa Nane wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, alisema serikali yake itazingatia haki na usawa.

Alisema lengo lake ni kujenga Zanzibar bila kujali tofauti za kiitikadi na kuahidi kuyaenzi maridhiano yaliyo katika Katiba na kushirikiana na vyama vingine kuijenga Zanzibar kwa kuwa ni kubwa na muhimu kuliko tofauti za kisiasa.

"Uchaguzi umekwisha tushirikiane kuiletea maendeleo nchi yetu, kila mmoja ana wajibu wa kufanyakazi na kutambua mchango wake ni muhimu kwa maendeleo ya nchi nchi yake," alisema.

"Serikali nitakayoiunda itaongozwa kwa misingi ya haki, uwajibikaji, uwazi na usawa kwa wananchi wote bila kumbagua mtu yeyote kutokana na itikadi yake, jinsia au eneo analotoka, sote ni wamoja na tunahaki ya kunufaika na huduma na rasilimali zetu kwa misingi ya usawa," alisema.

Dk. Mwinyi, alitoa ahadi hiyo muda mfupi baada ya kuapishwa na Jaji Mkuu wa Zanzibar, Omar Othman Makungu, katika sherehe zilizofanyika Uwanja wa Amani na kuhudhuriwa na viongozi wa kitaifa akiwamo Makamu wa Rais wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano, Samia Suluhu Hassan.

Pia, alisema atahakikisha anaendeleza pale alipoishia Rais mstaafu, Dk. Ali Mohamed Shein na kumshukuru kwa hekima zake na busara alizozitumia wakati wote tangu alipoteuliwa kugombea wadhifa huo.



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akihutubia baada ya kuapishwa jana. **PICHA: IKULU**

Rais Dk. Mwinyi aliahidi kushirikiana na viongozi na wananchi kuleta maendeleo ya Zanzibar na kuwataka Wazanzibari kudumisha amani na umoja wa kitaifa ili kufikia malengo ya maendeleo pamoja na kuleta mapinduzi ya uchumi wa Zanzibar.

"Nakusudia kuunda serikali makini yenye utendaji kazi bora, yenye kuwajibika kwa wananchi na kuchagua viongozi waadilifu ili kufikia malengo ya kuleta maendeleo ya haraka kwa wananchi wa Zanzibar."

Hata hivyo, alisema anakusudia kuelezea mwelekeo wa Serikali ya Awamu ya Nane atakapokuwa akizindua Baraza la Wawakilishi na kusisitiza kuunda serikali yenye uwezo wa kujenga misingi ya uwajibikaji yenye kupiga vita ubadhilifu ili kuharakisha maendeleo ya Zanzibar pamoja na kuondoa kero zinazowagusa wananchi kwa kuhakikisha viongozi wanashuka kushughulikia matatizo ya wananchi.

Awali, Dk. Mwinyi alitoa salamu kwa Rais mteule wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. John Magufuli ambaye amewatakia kheri na fanaka wananchi wa Zanzibar kwa kukafanikisha uchaguzi mkuu kwa amani na kujitokeza kwa wingi kwenye sherehe za kuapishwa rais mpya wa Zanzibar.

Viongozi wengine waliohudhuria sherehe hiyo ni Makamu wa Pili wa Rais mstaafu, Balozi Seif Ali Iddi, Rais msaatafu Ali Hassan Mwinyi, Rais mstaafu Amani Abeid Karume, Rais mstaafu Jakaya Kikwete, Waziri Mkuu Kasim Majaliwa, Makamu Rais mstaafu, Dk. Mohammed Gharib Bilali, Waziri kiongozi mstaafu Shamsi Vuai Nahodha pamoja na wawakilishi wa vyama rafiki vya CCM kutoka Zimbabwe, Namibia, China, Uganda, DR Congo, Afrika Kusini, Msumbiji, Kenya na wawakilishi wa baadhi ya mabalozi wa Tanzania kutoka mataifa ya nje.

**MAMIA WAJITOKEZA KUSHUHUDIA**

Mamia ya wananchi wa Zanzibar walijitokeza kushuhudia kuapishwa kwa Rais mpya wa Zanzibar, Dk. Mwinyi licha ya kiongozi wa upinzani Zanzibar kupitia Chama cha ACT- Wazalendo, Maalim Seif Sharif Hamad, kususia sherehe hizo.

Wananchi hao walianza kujitokeza majira ya saa 12 asubuhi, huku wananchi kutoka Kisiwani Pemba waliwasili toka juzi kwa meli na kupokelewa kwa mabasi maalum katika Bandari ya Malindi.

Hali ya usalama ilikuwa ya utulivu huku magari yaliyokuwa na askari wenye silaha, wakiwamo polisi na askari wa vikosi vya SMZ, wakiendelea kufanya doria katika mitaa mbalimbali ya mjini Zanzibar.

Sherehe hizo zilitanguliwa na gwaride maalum la kumuaga Rais mstaafu Dk. Ali Mohamed Shein.

Mizinga 21 ya heshima kwa rais mpya ilipigwa na baadaye alikagua gwaride la vikosi vya ulinzi na usalama kiwanjani hapo huku kukiwa na hali ya hewa ya mawingu na jua.

Viongozi wa dini walitangulia kwa kusoma dua maalum ya kumwombea kheri na uongozi bora rais mpya akiwamo Askofu wa Kanisa Katoliki Jimbo la Zanzibar Agostio Shao, Askofu wa Kanisa la Anglikana Dayosisi ya Zanzibar, Michael Hafidh na Naibu Kadhi Mkuu wa Zanzibar Sheikh Hassan Othman Ngwali.

**KIAPO CHA UAMINIFU**

"Mimi Hussein Ali Mwinyi naapa kwa jina la Mwenyezi Mungu kwamba nitakua mwaminifu kwa Zanzibar na kuitumikia kwa moyo wangu wote na kwamba nitaihifadhi, nitailinda na kuitetea Katiba ya Zanzibar na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na watu wake kwa mujibu wa sheria iliyowekwa nakuomba Mwenyezi Mungu unisaidie."

"Mimi Hussein Ali Mwinyi naapa kwamba nitatekeleza kazi zangu za urais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa uadilifu na kutimiza wajibu wangu kwa moyo mkunjufu na kwamba nitawatendea haki watu wote kwa mujibu wa Katiba na sheria na nikiongozwa na haki, mila na desturi ya Zanzibar bila ya kushawishiwa, woga wala chuki nakuomba Mungu unisaidie."

Awali, shangwe ziliibuka viwanjani hapo baada ya Rais mstaafu Jakaya Kikwete kuingia kwenye viwanja hivyo.

Kikosi cha makomandoo kiliibua shangwe wakati wakipita mbele ya Rais mpya wa Zanzibar wakiwa wamebeba mabegi yenye mizigo mizito na wengine wakipita kwa mwendo wa kikomandoo.

## Vigogo CHADEMA kufunguliwa mashtaka tuhuma za kigaidi

**Na Elizabeth Zaya**

JESHI la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, limesema litawafungulia mashtaka ya kigaidi viongozi wa Chama cha Demokrasia ya Maendeleo (CHADEMA), kwa tuhuma za kupanga njama za kufanya maandamano na kushawishi watu kuingia barabarani bila kibali.

Akizungumza katika studio za ITV, Mikocheni jijini Dar es Salaam, Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Kamishna Mwandamizi, Lazaro Mambosasa, alisema miongoni mwa viongozi waliokamatwa ni Mwenyekiti wa chama hicho taifa, Freeman Mbowe, na aliyekuwa Meya wa Ubungo, Boniface Jacob.

Wengine ni aliyekuwa Mbunge wa Arusha Mjini, Godbless Lema, pamoja na vijana ambao walishawishiwa kuendesha maandamano hayo, Abwines Kichengwa, Elisha Mangauka na Godfrey Mkandala ambaye ni msaidizi wa aliyekuwa Mbunge wa Kawe, Halima Mdee na mwingine aliyemtaja kwa jina moja la Isack.

Mambosasa alisema jeshi hilo linaendelea kuwafuatilia viongozi wengine ambao wametoka katika mikoa yao walikokuwa wakigombea na kukimbilia Dar es Salaam, akiwamo aliyekuwa Mbunge wa Mbeya Mjini, Joseph Mbilinyi kwa jina maarufu Sugu.

Mambosasa alisema viongozi hao walikamatwa wakiwa katika vikao mbalimbali vya kupanga mikakati ya kufanya maandamano bila kibali na kuwahamasisha watu kuingia barabarani kufanya vitendo vya uvunjifu wa amani.

Alisema miongoni mwa vitu ambavyo viongozi hao walikuwa wanapanga ni pamoja na kushawishi watu kuingia barabarani, kuchoma vituo vya mafuta, magari, ofisi za serikali na za wapinzani wao, miundombinu na kuchoma masoko, matairi barabarani kufunga njia.

"Mbowe na wenzake watashtakiwa kwa makosa ya ugaidi kwa sababu kupanga kulipua vituo vya mafuta, kuchoma masoko, ofisi, na kupanga kuharibu miundombinu, hivyo ni uharibifu mkubwa na ni vitendo vya ugaidi na hapa ndipo uharamu wa maandamano ulianzia na pia hawakutoa taarifa kwa Jeshi la Polisi, na ndiyo maana tulikataza kwa sababu hayakuwa ya amani," alisema Mambosasa.

"Na jambo la kushangaza ni kwamba watu wametoka kwenye maeneo yao ambako walishindwa katika uchaguzi, wamekimbilia Dar es Salaam kuja kuanzisha fujo na vitendo vya uvunjifu wa amani. Jana (juzi) tulikuwa na watuhumiwa wanne, na leo (jana) wameongezeka wengine watatu na tunaendelea kuwakamata wengine."

Mambosasa alisema Jeshi la Polisi limejipanga kuhakikisha kwamba uamuzi uliofanywa na wananchi katika sanduku la kura unalindwa.

"Uchaguzi umeisha na tayari Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), ilishatoa maelekezo kwamba mtu yeyote ambaye hajaridhika apeleke malalamiko na kufuata sheria, na najua viongozi hawa ni wasomi na wanafahamu njia sahihi za kufuata, lakini kwa sababu wanajua nini wanakitafuta wanaamua kuingia barabarani," alionya Mambosasa.

"Nawaomba wananchi wote wa Dar es Salaam kuwa makini na kutoa taarifa ya kile kinachoendelea, na tumejipanga vizuri kudhibiti kinachopangwa na magenge hayo kufanya uharamu wa hayo maandamano."

Mambosasa alisema wamejipanga kuhakikisha kila anayepanga kufanya maandamano hayo anakamatwa kabla ya kukamilisha azma hiyo.

"Na anayeingia barabarani ni kwa risk (jihatarisha) yake mwenyewe, na hatatoka salama kwa sababu sisi tumejipanga. Kilichofanyika kupitia sanduku la kura ni maamuzi ya mwananchi na huwezi kuwaamulia na ni lazima yaheshimiwe na tuko tayari kuhakikisha kwamba maamuzi hayo yanalindwa."

Aliwataka vigogo wote walioshindwa katika majimbo yao warudi walikotoka badala ya kukimbilia Dar es Salaam kupanga mbinu ovu za uvunjifu wa amani.

"Walioshindwa warudi majimboni kwao kwa sababu hawajashindiwa hapa Dar es Salaam na kitendo cha kuwa hapa ni uchokozi wa dhahiri na tungependa tubaki na waliokuwa wanagombea nafasi zao, kama hawajaridhika wafuate utaratibu wa kwenda tume au mahakamani, lakini kitendo cha kutoka nje ya mfumo huo wa kisheria," alisema Mambosasa.

Mambosasa alisema katika kudhibiti maandamano hayo, jeshi hilo limeshirikiana na wadau mbalimbali wa ulinzi ikiwamo vyombo vya ulinzi na usalama vya kampuni binafsi.

"Hivi ninavyosema operesheni inaendelea na tumejipanga vizuri, tuna vikosi vya FFU, vikosi vya polisi kutoka katika wilaya 13 za kipolisi ambazo zinaongozwa na wakuu wa polisi wa wilaya hizo, tumeweka utaratibu wa vijana makachero, polisi wa doria, wanaofuatilia mikutano ya chini kwa chini inayofanyika kwa siri kwa ajili ya kukusanya taarifa za wahuni wanaopanga hujuma," alisema Mambosasa.

"Pia tuna vikundi vya ulinzi shirikishi na polisi kata ambao wanafuatilia mwenendo wa hao watu."

Mambosasa alisema mpaka jana walikuwa hawajapata jaribio lolote la kutekeleza mipango ya uharibifu iliyokuwa imepangwa na waandamanaji hao.

"Jiji liko shwari, barabara ziko wazi na hatujapata jaribio lolote la kuyataekeleza yale yote yaliyokuwa yamepangwa kutekelezwa, na sitegemei kutokea kwa sababu tupo kwenye ground," alisema Mambosasa.

Kadhalika, alisema wanaendelea kuwatafuta watu wengine wanaopanga kufanya maandamano hayo na kitakachofuata ni kukamilisha taratibu la jalada kwenda kwa mwanasheria kabla ya kuwafikisha mahakamani.

HABARI KITAIFA

# Ahmadiyya yapongeza uchaguzi wenye utulivu

**Na Peter Mkwavila,**

DODOMA

JUMUIYA ya Ahmadiyya Musilim Jamaat Tanzania imeipongeza Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) na Watanzania kwa kufanikisha zoezi la upigaji kura lililofanyika kwa uhuru, haki, utulivu na amani.

Pongezi hizo, zimetolewa na Shekhe Bashart Rehman Butt, jijini hapa wakati akizungumza na waandishi wa habari, ambapo alisema NEC, imefanikisha kwa kiasi kikubwa na kuwawezesha Watanzania kufanya uchaguzi huo kwa utulivu, amani, haki na huru.

Shekhe Butt alisema kuwa NEC iliweka utaratibu mzuri ambao ulitoa fursa kwa wapigakura kujitokeza kwa wingi na kufanikisha kuwa na amani na utulivu.

Aliwapongeza Watanzania kwa kujitokeza ili kutimiza haki yao ya msingi ya kupiga kura na kufanikisha kuwachagua viongozi wanaowataka.

"Ni matumaini yangu kwa viongozi watakaochaguliwa na Watanzania watakuwa bora, kwa kuwa wamechaguliwa kwa lengo la kuwatumikia Watanzania wote kwa uzalendo bila kujali itikadi yoyote ya kichama," alisema.

Aliwataka Watanzania baada ya kufanyika uchaguzi huu watoe ushirikiano na viongozi waliochaguliwa bila kujali itikadi ya vyama vyao vya siasa.

"Baada ya uchaguzi huu ninawaomba Watanzania kufanya kazi kwa bidii, ili serikali iweze kufanikisha zaidi kwa yale ambayo yaliyokuwa yakiahidiwa na wagombea kwenye mikutano ya kampeni," alisema.



Makomandoo kutoka Jeshi la Wananchi wakipita mbele ya Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi baada ya kuapishwa jana. **PICHA: IKULU**

# Lipumba atoa msimamo wa CUF kutoshiriki uchaguzi mkuu

**Na Elizabeth Zaya**

CHAMA cha Wananchi (CUF), kimesema hakitashiriki tena katika Uchaguzi Mkuu mpaka itakapopatikana Tume Huru ya Uchaguzi wa Tanzania.

Pia, chama hicho kimesema hakikubaliani na matokeo yaliyotangazwa katika uchaguzi mkuu uliofanyika Oktoba 28, mwaka huu, kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Zanzibar.

Kwa mujibu wa CUF, uamuzi huo umetokana na Kamati ya Uongozi ya Baraza Kuu la Uongozi la Taifa na Kamati ya Utendaji ya Taifa ya chama hicho iliyofanya kikao cha pamoja cha dharura kutathmini mwenendo na matokeo ya uchaguzi huo, Novemba 2, mwaka huu.

Akitoa tamko hilo jijini Dar es Salaam jana, Mwenyekiti wa chama hicho, Profesa Ibrahim Lipumba, alisema kuanzia sasa kwa kushirikiana na wadau wengine, kitajikita katika kuwahamasisha Watanzania kwa njia mbalimbali kupigania Katiba mpya yenye misingi ya demokrasia na utawala bora.

Profesa Lipumba alisema chama hicho kimepanga kufanya maombi maalum siku ya Alhamisi wiki hii.

"Tunawaomba Watanzania wote wanaopenda haki nchini kote, kufanya ibada maalum siku ya Alhamisi, kwa kufunga kula mchana na kufanya dua na maombi baada ya kufungua, kila mtu kwa imani yake," alisema Profesa Lipumba.

"Dua na maombi yatajikita kumwomba Mwenyezi Mungu kupitisha hukumu ya haki juu ya kile kilichotendeka katika uchaguzi mkuu wa 2020."

Vile vile, Profesa Lipumba alisema chama hicho kitaanzisha mazungumzo na Jumuiya za Kimataifa, kuiomba kuisaidia Tanzania kujenga misingi ya kudumu ya demokrasia na utawala bora.

# Maandalizi kumwapisha Magufuli yapamba moto

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imeendelea kuandaa mazingira ya kuapishwa kwa Rais mteule Dk. John Magufuli, ambaye ataapishwa Alhamisi katika Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma.

Nipashe imetembelea eneo la kuzunguka uwanja huo na kushuhudia vikosi mbalimbali vya jeshi vikiingia ndani ya uwanja huo, kufanya mazoezi ya kijeshi na ndege zikifanya mazoezi angani kwa ajili ya sherehe ya kuapishwa kwake.

Pamoja na mazoezi hayo, pia barabara za kuzunguka uwanja huo zimejengwa kwa kiwango cha lami ambapo awali zilikuwa za changarawe.

Kadhalika, baadhi ya maduka yaliyopo kwenye uwanja huo yameanza kufungwa ili kupisha shughuli hiyo, huku katika uwanja wa Barafu yakijengwa mahema kwa ajili ya wananchi kukaa, ambao hawataingia ndani ya uwanja wa Jamhuri.

Akizungumza kuhusu ulinzi kuimarishwa, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, Gilles Muroto, alisema wamejiandaa kikamilifu katika kuwapokea wageni wanaotarajiwa kuingia muda wowote kuanzia sasa kwa ajili ya sherehe hiyo.

Muroto alisema hali ya usalama kwa sasa ni shwari, na wanaendelea kufanya doria mbalimbali za miguu, magari na kwa kutumia mbwa, ili kuimarisha ulinzi wakati wote wa maandalizi na kuapishwa kwa Rais huyo mteule.

Juzi, Msemaji Mkuu wa Serikali, Dk. Hassan Abbas, alisema serikali itaendelea kutoa taarifa ya viongozi wa kimataifa watakaohudhuria sherehe hiyo, na atatoa orodha yao hivi karibuni kabla ya siku ya kuapishwa Novemba 5, mwaka huu.

"Kwa sasa tunaendelea na taratibu za maandalizi ya uapisho uwanja wa Jamhuri, hadi sasa upo tayari takribani asilimia 95 na sherehe itahudhuriwa na viongozi mbalimbali wa kitaifa na kimataifa, ambao katika siku mbili tatu zijazo nitatoa orodha kamili ya viongozi wa kimataifa watakaokuwapo," alisema.

Alisema viongozi kadhaa wameshathibitisha kuwapo kwenye uapisho huo na zitapambwa na burudani mbalimbali ikiwamo wasanii wa mziki wa kizazi kipya, ngoma na vikundi vya asili.

"Wananchi watakaohudhuria wa Dodoma na mikoa jirani niwaombe sana kufikia saa moja kamili asubuhi wawe wamefika uwanjani na kuketi eneo watakaloelekezwa," alisema.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Mtaa wa Oysterbay jijini hapa, Elizabeth John, alisema wamejipanga kuhudhuria tukio hilo ambalo kwa Dodoma linafanyika kwa mara ya kwanza.

Naye, Omary Athumani alisema kumekuwa na matangazo ya kuhamasisha wananchi kujitokeza kwenye sherehe hizo, na kwamba watahakikisha wanahudhuria kwa wingi kwa kuwa ni mara yao ya kwanza Dodoma kushuhudia uapisho.

"Tumeshuhudia sherehe za Uhuru, za Muungano, lakini za uapisho ndio mara ya kwanza, hivyo tutahudhuria kwa wingi kushuhudia Rais wetu akiapishwa," alisema.

# CCM yaita wagombea uspika, unaibu, mameya na wenyeviti

**Na Christina Mwakangale**

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM), kimetangaza kuanza kupokea maombi ya wanaowania nafasi ya uspika na naibu spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Pia, kimesema kitapokea maombi ya mameya wa jiji, halmashauri, manispaa pamoja na wenyeviti wa halmashauri.

Katibu wa Itikadi na Uenezi wa chama hicho, Humphrey Polepole, aliyasema hayo jana katika taarifa aliyotoa kwa umma.

Alisema baada ya kukamilika mchakato wa uchaguzi mkuu na sasa ni wakati wa kuwapata wawakilishi kulingana na katiba, kanuni na sheria za nchi.

"Jukumu la CCM ni kuanza kupanga safu ya uongozi katika vyombo vya uwakilishi. Kwa mujibu wa sheria chama kinaalika wanachama wenye sifa wanaoomba wafikiriwe na chama katika nafasi ya uspika wa bunge, naibu spika, meya wa halmashauri ya jiji au manispaa na wenyeviti wa halmashauri wilaya," alisema Polepole.

Alibainisha kwamba pamoja na sifa za wanaoomba nafasi hizo, sheria za nchi zinawataka waombaji wote lazima wawe wamekidhi sifa za uongozi kwa mujibu wa Katiba ya CCM ya Mwaka 1977, Toleo la Mwaka 2020, ikisomwa pamoja na Kanuni ya Maadili na Uongozi Toleo la Mwaka 2012.

Polepole aliongeza kuwa fomu za wanaoomba nafasi ya uspika na naibu spika zinapatikana makao makuu ya chama hicho jijini Dodoma, Lumumba na ofisi kuu iliyopo Kisiwandui, Zanzibar.

Kadhalika, alisema wanaoomba nafasi ya uenyekiti kwenye halmashauri fomu zinapatikana kwenye ofisi za chama hicho wilaya.

"Tarehe ya kuchukua na kurejesha fomu zote tajwa ni leo (jana) Novemba 2, mwaka huu, hadi saa 10 jioni na kurejesha ni leo saa 10 jioni," alisema Polepole kwenye taarifa hiyo.

Alieleza kuwa mapendekezo ya kamati za siasa za wilaya na mkoa yawe yamefika ofisi ya Katibu Mkuu, Novemba 6, mwaka huu, baada ya kamati za siasa za halmashauri kuu za wilaya kutoa mapendekezo kwenye kikao kitakachoketi kesho.



Baadhi ya masanduku yaliyotumika kupigia kura kwenye uchaguzi mkuu uliopita yakiingizwa kwenye lori kutoka ukumbi wa Anatoglo jijini Dar es Salaam. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**.

# Adaiwa kuua mke, shemeji kwa shoka

**Na Restuta Damian,** BUKOBA

JESHI la Polisi mkoani Kagera linamshikilia Faraji Yunus (44), mkazi wa Kijiji cha Kikagati wilayani Muleba mkoani Kagera, kwa tuhuma za mauaji ya mkewe na shemeji kwa shoka.

Anadaiwa kuwaua mkewe, Nadia Coroneli (35) na shemeji yake, Shadia Yunusu (25), wakazi wa kijiji hicho. Kamanda wa Polisi mkoani Kagera, Revocatus Malimi, alisema kuwa Oktoba 29, mwaka huu majira ya saa 12 jioni, mtuhumiwa akiwa kijijini hapo alisababisha ugomvi uliosababisha mauaji hayo.

Kamanda alisema, mtuhumiwa alipata taarifa kuwa mkewe alikuwa akifanya usaliti wa ndoa na kufikia hatua ya kutaka kwenda kuolewa sehemu nyingine, hivyo mtuhumiwa kuanza matukio ya kuzua ugomvi.

"Alipopata taarifa hizo alianza ugomvi na mkewe, ambao ulisababisha kumuua mkewe Nadia na Shadia Yusuph, mke wa mdogo wake Yusuf Yunusu kwa kutumia shoka," alisema Kamanda Malimi.

Aidha, alisema akiwa katika ugomvi huo, alifika mtu ambaye mtuhumiwa alikuwa akidai kuwa ana mahusiano na mkewe, na kutaka kuamulia ugomvi huo.

Kamanda alisema mtuhumiwa alimuua shemeji yake kutokana na kumtuhumu kuwa alikuwa anamtafutia mabwana mkewe, huku akijua kuwa ni mke wake wa ndoa.

Alisema baada ya tukio hilo, mtuhumiwa aliharibu kukimbia, lakini juhudi za polisi wilayani Muleba ziliwezesha kukamatwa na kufikishwa kituoni.

Alisema, upelelezi wa tukio hilo, unaendelea ili kubaini sababu zaidi kabla ya kufikishwa mahakamani.

## Majengo ya serikali yachomwa, magari yaharibiwa kisa uchaguzi

**Na Said Hamdani,** LINDI

BAADHI ya wananchi wenye hasira mkoani Lindi, wanadaiwa kufanya uharibu wa mali za umma ikiwamo kuchoma majengo ya serikali, binafsi na vyombo vya usafiri kama magari, pikipiki na kusababisha hasara kubwa.

Hata hivyo, hasara halisi ya uharibifu huo, inadaiwa kusababishwa na mambo ya kisiasa.

Mkuu wa Mkoa huo, Godfrey Zambi, ameyaeleza hayo mjini Lindi, alipokuwa akitoa taarifa kwa waandishi wa habari kuhusiana na uharibifu uliofanywa wakati wa uchaguzi mkuu Oktoba 28, mwaka huu.

Watu hao wanadaiwa kufanya fujo kwa sababu ya kutoridhishwa na mwenendo wa uchaguzi ulivyokwenda, kutokana na kile kinachodaiwa kuhujumiwa, ikiwamo kuzuiliwa mawakala kuingia vituoni, ongezeko la vituo hewa vilivyo nje ya mfumo na vitambulisho vya kupigia kura.

Madai mengine ni kubadilishiwa matokeo ya ushindi ya mgombea aliyeshinda kupewa mgombea wa Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Zambi alisema katika fujo hizo, magari zaidi ya saba kati ya hayo mawili ya polisi, majengo ya serikali pamoja na binafsi tisa na pikipiki moja, yaliharibiwa kwa kuchomwa moto.

Zambi alizitaja wilaya zilizoathirika kutokana na uharibifu huo ni Liwale, Nachingwea, Kilwa na Lindi katika Halmashauri ya Mtama.

Amesema Liwale magari zaidi ya saba, likiwamo la polisi na binafsi yaliyokodiwa kusaidia uchaguzi huo, yaliharibiwa, na kwamba nyumba mbili na magari matatu ya Mbunge mteule, Mohamed Kuchauka.

Imo pia zahanati ya Diwani mteule Kata ya Liwale Mjini, Omari Mkoyage na nyumba moja ya askari polisi.

Zambi alisema wilayani Nachingwea, magari matatu na nyumba, mali za Diwani mteule Ahamadi Makoroganya, gari moja la polisi na nyumba zimechomwa moto, huku jengo la Mahakama Wilaya limenusurika licha ya kuwamo kwenye orodha ya kutaka kuichoma.

Kwa mujibu wa Zambi, Halmashauri ya Mtama, watu hao walichoma moto majengo mawili, ikiwamo ofisi ya muda anayoitumia Mkurugenzi Mtendaji, Samuel Waryoba, Ofisi ya Serikali ya Kata ya Mtene na jengo la saluni la mtendaji wa kata hiyo.

Alisema Jeshi la Polisi linawashikilia watu kadhaa kwa ajili ya mahojiano, kwa lengo la kuwabaini waliohusika.

# Anayetuhumiwa kupora sanduku la kura asakwa

**Na Said Hamdani, LINDI**

MKUU wa Wilaya ya Lindi, Shaibu Ndemanga, amesema serikali inaendelea kumtafuta kijana anayedaiwa kukimbia na sanduku la kupigia kura wiki iliyopita katika Kata ya Madangwa, Jimbo la Mtama ili sheria iweze kuchukuwa mkondo wake.

Ndemanga alibainisha hayo alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari, na kuthibitisha kuwapo kwa tukio la kijana ambaye hata hivyo hakumtaja jina, kupora moja ya masanduku ya kupigia kura na kutokomea nalo kusikojulikana.

"Ni kweli tukio la kuporwa kwa sanduku moja la kupigia kura kati ya matatu yaliyokuwapo kwenye kituo limetendeka," alisema Ndemanga.

Alisema wanaendelea kumsaka kisha kumfikisha kwenye vyombo vya sheria.

"Tayari taarifa zake tunazo na tunakuhakikishieni ndugu waandishi muda si mrefu atatiwa mikononi," alisema.

Ilidaiwa kuwa kijana huyo alifika kituoni hapo na kupiga kura na alipomaliza kutumbukiza shahada katarasi yake, alipora sanduku lenye kura za udiwani kisha kutokanalo nje na kupanda pikipiki na kutokomea nalo kusikojulikana. Huku ndani yake likiwa na kura kadhaa zilizoshapigwa.




Mchuuzi wa biashara ya matikiti akiandaa matunda hayo kando ya barabara ya Nyerere jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Vibaka wadaiwa kutumia nyembe kupora

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAAKAZI wilayani Kahama mkoani Shinyanga, wameliomba Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na wenyeviti wa serikali za mitaa kukomesha wimbi la vibaka ambalo limekuwa likiwapora watu nyakati za usiku.

Wakizungumza na gazeti hili kwa nyakati tofauti, walisema kuwa asilimia 80 ya nyumba za Kahama zimetobolewa madirisha na ukikutana nao usiku ukiwa huna fedha kama mwanamke wanakulazimisha kufanya nao ngono.

Juma Swed, mkazi wa Kata ya Mhongolo, alisema kumeibuka wimbi la vibaka katika kata za Nyahanga Shunu, Malunga, Mhongoro na Nyihogo ambao wamekuwa wakiwapora wananchi wanaokutana nao nyakati za usiku wakirejesha nyumbani.

Naye Mwajuma Hamisi, alisema vibaka hao wamekuwa wakitembea makundi kwa makundi, na unapokutana nao kama huna chochote hasa fedha wanakuchangaraka viwembea na kukuchukulia simu na mkoba.

"Tatizo kama hili kipindi cha nyuma lilikithiri na lilitatuliwa kwa wakati, na watu tuliendelea na shughuli zetu," alisema na kuendelea:

"Ila sasa limeibuka tena, na safari hii kwa kinamama tunaokamatwa usiku hatuna fedha... tumekuwa tukicharangwa viwembe na kunyang'anywa simu na mkoba," alisema.

Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Mhongolo, Emmanuel Nangale, alisema matukio ya namna hiyo kwa kipindi cha nyuma yalikuwa yamekithiri, lakini kwa kipindi cha miezi miwili nyuma yameibuka kwa kasi na wanajipanga kuyatatua.

Aliwataka wakazi wa kata hizo kuhakikisha wanatoa taarifa kwenye ofisi za serikali za mitaa na kituo cha polisi endapo watakutana na kundi la vijana na kufanyiwa vitendo vya kikatili.

Kamanda wa Polisi mkoani Shinyanga, Debora Magiligimba, alisema ofisi yake haina taarifa juu ya wimbi la vibaka wanaopora wananchi nyakati za usiku, na kama lipo atahakikisha analifuatilia kwa karibu na kulichukulia hatua stahiki.

## Wakulima, wavuvi wahakikishiwa masoko

**Na Richard Makore,** MWANZA

WAKULIMA na wavuvi katika mikoa sita ya Kanda ya Ziwa wamehakikishiwa soko la mazao yao pamoja na samaki wanazovua katika Ziwa Victoria.

Kauli hiyo ilitolewa jana jijini Mwanza na Meneja wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB), Kanda ya Ziwa, Mike Granta, alipozungumza na Nipashe.

Granta alisema katika kuendeleza kilimo, TADB imetoa Sh. bilioni 40 kwa vyama vikuu ya ushirika mkoani Kagera ili kuwaendeleza wakulima.

Alisema fedha hizo ni kwa ajili ya kununua mazao ya wakulima hao, kupitia ushirika wao ili kuhakikisha kwamba wanakuwa na soko la uhakika.

Aliongeza kuwa miaka ya nyuma wanunuzi binafsi walikuwa wananunua mazao ya wakulima ikiwamo kahawa kwa bei ndogo, lakini baada ya TADB kutoa fedha hizo kwa vyama vya ushirika, sasa wanalipa bei nzuri.

Meneja huyo alisema mpaka sasa asilimia kubwa ya kahawa na pamba inauzwa nje ya nchi, na kwamba sehemu kidogo inayobaki inauzwa nchini.

Katika kuhakikisha TADB inaendeleza kilimo, Granta alisema katika Kanda ya Ziwa wametoa mikopo ya matrekta zaidi ya 50 yenye riba nafuu ili kuhakikisha wakulima wanalima kwa tija.

Kuhusu bei ya pamba waliyokuwa wanalipwa wakulima, alisema wamefanikiwa kuongeza bei kutoka Sh. 814 kwa kilo hadi Sh. 900 ili kuhakikisha wakulima wanapata bei nzuri.

Alisema ili kuhakikisha wanakuza kilimo, TADB pia inafufua baadhi ya viwanda vya kuchambua pamba.

Aliongeza kuwa licha ya juhudi mbalimbali zinazofanywa na TADB kuwasaidia wakulima Kanda ya Ziwa, bado kundi hilo linakabiliwa na kikwazo cha kutegemea kilimo cha kusubiri badala ya kile cha umwagiliaji.

Akizungumzia sekta ya uvuvi ambayo pia inajumuishwa kwenye kilimo, Granta alisema, wametoa mikopo kwa vyama mbalimbali vya wavuvi pamoja na viwanda vya kuchakata minofu.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# *Kila la heri Mwinyi, sasa wakati kutibu majeraha uchaguzi*

**JANA** Rais mpya wa Awamu ya Nane wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, alikula kiapo cha kuongoza visiwa hivyo kwa miaka mitano.

Kiapo hicho ni baada ya kuibuka mshindi kwa kupata kura 380,402 sawa na asilimia 76.27 kati ya wagombea 16 wa vyama vya upinzani walioshiriki uchaguzi huo.

Baada ya kuapishwa, Dk. Mwinyi aliahidi kuunda serikali itakayoenzi maridhiano ya kitaifa kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, na marekebisho yake.

Tunampongeza Rais Mwinyi kwa kushika usukani wa kuiongoza Zanzibar, lakini ndiyo wakati mwafaka wa kuijenga nchi yenye umoja katika kuondoa tofauti zilizojitokeza wakati wa uchaguzi mkuu.

Kauli hiyo inakuja siku chache tangu kufanyika kwa uchaguzi mkuu wa Oktoba 28, mwaka huu, ambao pamoja na mafanikio yake chama kikuu cha upinzani visiwani humo, ACT-Wazalendo, kilikataa kuyatambua matokeo hayo na baadhi ya viongozi wake wanashikiliwa na Jeshi la Polisi kwa kufanya maandamano.

Kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2010 na kuruhusu uwapo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa, inataka mgombea urais aliyemkaribia mshindi kwa idadi ya kura nyingi ashirikishwe katika serikali hiyo.

Jambo hilo lilifanyika wakati wa serikali ya awamu ya saba chini ya Dk. Ali Mohamed Shein, ambaye Maalim Seif Sharif Hamad, alikuwa Makamu wa Kwanza wa Rais.

Kwa kauli ya Mwinyi na matokeo ya urais ambayo Maalim Seif alipata kura zaidi ya asilimia 19, huenda itatibu majeraha yaliyozalishwa na uchaguzi huo.

Katika hotuba yake aliahidi kushirikiana na wagombea wa vyama vingine vilivyokubali matokeo na kuheshimu maamuzi ya wananchi, huku akiahidi kushirikiana nao katika serikali atakayounda.

Tunaamini ni jambo jema sana kushirikiana katika kuimarisha Zanzibar katika kuhakikisha amani, upendo na ushirikiano unakuwapo.

Tunatarajia baada ya kuapishwa kuwa rais sasa atashughulikia yaliyojitokeza kwenye uchaguzi huo, ikiwa ni namna ya kuiponya Zanzibar dhidi ya mpasuko.

Ni dhahiri kuwa hakuna maendeleo yoyote yanaweza kufanyika katika eneo lisilo na maelewano na siku zote maelewano huliacha taifa likiwa moja na lenye nguvu kwa manufaa ya wote.

Hakuna ubishi kuwa uchaguzi umekwishwa na sasa ni wakati na kufanya maendeleo, na pia uchaguzi ni tukio la muda mfupi ambalo huja na kuondoka, lakini maisha ya watu yapo siku zote.

Kuna umuhimu mkubwa wa kurudisha umoja miongoni mwa Wazanzibari, ili kusiwe na ubaguzi kulingana na itikadi za kisiasa, ambazo wakati wa kampeni zilionekana wazi.

Sasa si wakati wa kuzodoana au kuzomeana ni wakati wa kutibu majeraha yaliyoachwa kwenye mioyo ya Wazanzibari, na ili kufanikisha nia kuwa na taifa moja ambalo litafikiria maendeleo.

Tunaamini majeraha ya uchaguzi yakitibiwa vyema kutakuwa na mwanzo mzuri wa kuwa na taifa imara na madhubuti kwa maendeleo ya wote bila kujali waliopiga kura ya ndiyo kwa rais aliyepo madarakani na waliochagua na kujionyesha kuwa ni wapinzani.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Christina Mwakangale

# *TEHAMA inakupa taarifa, lakini changamoto hudhalilisha*

**TEKNOLOJIA** ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), licha ya kukua kwa kasi imeleta mapinduzi ya upatikanaji taarifa mahali popote kwa urahisi duniani lakini, zikiibuka changamoto lukuki hasa wizi na udhalilishaji kinamama.

Aidha, inawezesha habari kupatikana kwa gharama nafuu kupitia simu za mikononi, zinazowawezesha watumiaji kupokea taarifa kutoka eneo lolote duniani baada ya kujiunga na kampuni tofauti za simu.

Mkuu wa kitengo cha usimamiaji, utekelezaji wa masharti ya leseni kutoka Mamlaka ya Mawasiliano (TCRA), Dk. Philip Filikunjombe, anasema TEHAMA imebadili mfumo wa mawasiliano katika sekta ya habari.

"Habari imekuwa jambo rahisi na mitandao ya kijamii inafikisha habari kirahisi. Wasikilizaji wanaongezeka kupitia redio na hata mtandaoni ingawa changamoto kubwa ni habari za picha za udhalilishaji wanawake," anasema Filikunjombe.

"Habari imefanya jambo jepesi na mitandao ya kijamii inasaidia kuzisambaza kwa urahisi. Wasikilizaji wanaongezeka ingawa changamoto ni udhalilishaji huku wanawake wakiathiriwa zaidi," anasema Filikunjombe.

Kukua kwa TEHAMA kunasababisha changamoto ikiwamo ongezeko la kesi za aina tofauti hasa za udhalilishaji kwenye kitengo cha huduma kwa wateja cha mamalaka hiyo.

Anasema changamoto nyingine ni kukua kwa habari feki, uhalifu mtandaoni zinazoletwa na kukosekana udhibiti wa mitandaoni ya kijamii.

Kitaaluma, picha isiyo na maadili haitumiwi, lakini mitandao ya kijamii mwanamama akikaa vibaya kwenye sherehe hiyo ndiyo inakuwa habari wanaipiga na kuisambaza mtandaoni," anasema Filikunjombe.

Filikunjombe anasema kanuni za maudhui mtandaoni za mwaka 2018, zinasaidia kujua watuma taarifa mtandaoni wanafahamika pia kuwawajibisha inapotakiwa au kuwataka wafanye marekebisho.

Kanuni hizo zinawahimiza wananchi kuwa kukiwa na uvunjifu wa kanuni waende polisi na si TCRA. Lakini masuala ya maudhui yanamtaka mtuma taarifa kuwalinda watoto pia kuwa na nywila kwenye akaunti za mitandao ya kijamii na simu za mikononi au kompyuta.

Ni wazi kuwa simu isiyo na nywila au neno la siri ikiibwa ni rahisi kufanyiwa uhalifu na kosa hilo adhabu yake ni faini isiyopungua Shilingi 5,000,000 au kifungo kisichopungua miezi 12.

Filikunjombe anasema kwenye dunia ya teknolojia kunaweza kuwa na kitendo kimoja na kuleta madhara tofauti kwa mfano mtu alipita nyumbani kwa jirani akakata waya na umeme ukakosekana.

Aidha, mwingine alikata waya kama huo hospitalini nayo ikakosa umeme, huduma za dharura na muhimu zikasimama, wawili hao wakikamatwa nani atapewa adhabu kubwa? Sheria inatoa maelekezo.

Anataja makosa mengine mtandaoni ni kuonyesha mbinu za kihalifu kama wizi, kutoroka gerezani, kuweka picha za mtoto mtandaoni, kukutwa na picha za utupu.

Filikunjombe anakumbusha kuwa ni marufuku kutumia habari za media nyingine bila idhini, lakini ni kosa.

Ofisa Mwandamizi Semu Mwakyanjala, anasema sekta ya habari na mawasiliano nchini, imeleta baadhi ya changamoto zikiwamo wizi wa mtandao na udhalilishaji wa kijinsia na kwamba ukuaji huo unahitaji usimamizi madhubuti ili isiwe hatari nchini.

Anasema vyombo vya habari katika mfumo wa kidigitali ikiwamo vya mtandaoni zinaelimisha ingawa zipo changamoto lakini zina mchango muhimu katika ujenzi wa taifa.

Anakumbusha kuwa kabla ya uhuru kulikuwa na vyombo vichache, lakini sasa kuna redio 183 kutoka moja baada ya uhuru na kwamba ni chanzo cha ajira kwa Watanzania.

Zipo televisheni 47 nchini na aidha, mfumo wa kutuma na kupokea pesa ni kitu kilichosambaa nchini na hivi sasa Watanzania milioni 27 wana akaunti benki kupitia mfumo wa mtandaoni na simu za mkononi.

TANGAZO

IPP

# PONGEZI



UONGOZI NA WAFANYAKAZI WA KAMPUNI ZA IPP WANAUNGANA NA WATANZANIA WOTE KUMPONGEZA MHESHIMIWA DK. HUSSEIN MWINYI KWA KUCHAGULIWA KUWA RAIS WA AWAMU YA NANE WA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI.

**HONGERA SANA.**

# HAFLA YA KUMWAPISHA RAIS ZANZIBAR



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akisalimiana na Rais mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mzee Ali Hassan Mwinyi, baada ya kuapishwa rasmi jana, katika hafla iliyofanyika Uwanja wa Amaan Zanzibar.



Rais wa Zanzibari, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akisalimiana na mkewe Mama Mariam Mwinyi baada ya kuapishwa rasmi na kushika wadhifa huo jana.



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akikagua gwaride maalum la vikosi vya ulinzi baada ya kuapishwa rasmi.



Dk. Hussein Ali Mwinyi akisalimiana na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, baada ya kuapishwa kuwa Rais wa Zanzibar jana.



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akisalimiana na Rais mstaafu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Amani Abeid Karume.



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akisalimiana na Waziri Kiongozi mstaafu wa Zanzibar, Shamsi Vuai. **PICHA: IKULU**




Mtoa huduma ya bima ya CHIF iliyoboreshwa ambaye jina lake halikupatikana akitoa maelezo kwa wateja waliofika kwenye banda hilo, lililopo eneo la Nyerere Square jijini Dodoma jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ujenzi wa jengo la ofisi wakamilika

**Na Waandishi Wetu**

UJENZI wa jengo la ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Madaba wilayani Songea mkoani Ruvuma ambalo limegharimu zaidi ya shilingi bilioni mbili, limekamilika na kuanza kutumika.

Mhandisi wa Halmashauri hiyo, Ludger Nchimbi, alisema ujenzi wa jengo hilo, ulianza rasmi mwaka 2017, na kwamba mradi umejengwa kwa awamu tatu.

Alisema katika awamu ya kwanza mkataba ulikuwa unatekelezwa na Mkandarasi Wakala wa Majengo Tanzania (TBA), ambao uligharimu zaidi ya Sh. milioni 493, awamu ya pili ni mkataba wa zaidi ya Sh. bilioni mbili na awamu ya tatu ujenzi umefanyika kwa force akaunti kwa ajili ya umaliziaji wa mradi huo.

"Tulipokea fedha kutoka serikali kuu bilioni tatu ambazo zimetumika kutoka mapato ya ndani, fedha iliyotumika mpaka kukamilika jengo hilo ni zaidi ya shilingi bilioni mbili," alisema.

Hata hivyo, alisema Mkandarasi TBA alisimamishwa kuendelea na kazi ya ujenzi na Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Christina Mndeme, Juni 6, mwaka huu, baada ya mkandarasi huyo kupata changamoto ya kufungiwa akaunti zake zote na kushindwa kuendelea na kazi, hali iliyosababisha halmashauri kutumia force akaunti kukamilisha mradi huo.

Alisema mradi wa jengo hilo kwa sasa umekamilika na tayari umeanza kutumika kuanzia Oktoba 21, 2020.

# Walimu wawachangia damu wajawazito

**Na Yasmine Protace,** MKURANGA

WALIMU wa shule za msingi katika Wilaya ya Mkuranga mkoani Pwani, wamejitolea kuchangia damu katika Hospitali ya Wilaya ya Mkuranga.

Lengo ni kuokoa maisha ya wajawazito wenye uhitaji wa damu pamoja na watoto.

Hayo yalisemwa na Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Ngunguti, Hamidu Nyombe, alipokuwa akizungumza na Nipashe baada ya kumalizika kwa utoaji damu units 10.

"Tumeamua kuchangia damu katika hospitali ya wilaya, lengo letu ni kuwasaidia wajawazito ambao wanafika hospitali na wanapokuwa na tatizo la kuongezewa damu, damu hiyo itatumika kuwasaidia," alisema.

Aliongeza kuwa damu hiyo pia itawasaidia hata watoto wenye uhitaji wa kuongezewa damu.

Mwalimu Nyombe alisema kuwa kutokana na kutolewa na damu, inaweza kutumika hata kwa waliopata ajali.

Alisema umoja wa walimu hao katika kipindi cha mwaka jana waliunga juhudi za Rais John Magufuli, ambapo wakichangia mifuko 120 ya saruji ili kuwezesha ujenzi wa vyumba vya madarasa katika maeneo mbalimbali.

Alisema mwaka huu, wamefanikiwa kutoa chakula, mavazi na virutubisho katika kituo cha watoto wenye uhitaji cha Malaika.

Aliongeza kuwa wanatarajia kujenga choo katika Shule ya Msingi Vikundi, ambacho kitawasaidia watoto wenye mahitaji maalum.

Kwa mujibu wa Mganga Mkuu wa Hospitali ya Wilaya Mkuranga, Dk. Stephen Mwandambo, kupatikana kwa msaada huo wa damu, utawasaidia wajawazito, watoto na waathirika wa ajali.

Aliwataka watumishi wengine kuwa na moyo wa kizalendo, huku akisisitiza uhitaji damu salama katika hospitali hiyo.

# H/shauri yaweka mikakati kumaliza uhaba madawati

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

HALMASHAURI ya Mji wa Kibaha mkoani Pwani, imesema imepanga mikakati ya kumaliza tatizo la uhaba wa madawati katika shule za msingi na sekondari.

Ofisa Uhusiano wa Halmashauri ya Mji wa Kibaha, Innocent Byarugaba, alibainisha hayo jana wakati akizungumza na Nipashe kuhusiana na mwenendo wa utengenezaji wa madawati na kuyasambaza kwenye shule.

Byarugaba alisema hadi kufikia Septemba 30, mwaka madawati 2,333 yametengenezwa kati ya 4,413 yanayohitajika kwa shule za msingi za halmashauri hiyo, ambapo 900 yametengenezwa kwa fedha za mapato ya ndani na 515 kwa kutumia kifungu cha ukarabati.

Alisema utengenezaji wa madawati hayo umezingatia idadi ya vyumba vya madarasa vilivyopo, na kwamba kwa sasa wamejipanga kumaliza upungufu wa madawati 2,080, ili kuendana na mahitaji ya wanafunzi.

Aidha, alisema kwa upande wa shule za sekondari hadi kufiki Septemba 30, mwaka huu madawati 1,206 yametengenezwa kati ya 2,000 yaliyokuwa yakihitajika.

Alisema kupitia chanzo cha mapato ya ndani, madawati 428 yalitengenezwa na mengine 500 kupitia kifungu cha ukarabati.

Mwanzoni mwa Septemba mwaka huu, Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Mhandisi Evarist Ndikilo, alitoa agizo kwa wakuu wa wilaya za mkoa huo kuhakikisha wanakamilisha zoezi la utengenezaji wa madawati, na kila shule kuwa na madawati kulingana na. mahitaji.

# Masheha sasa wapewa jukumu kesi udhalilishaji

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

MASHEHA wametakiwa kuzibeba kwa kuzifikisha polisi kesi za udhalilishaji wa watoto, ili kuondosha rushwa inayoweza kutendeka.

Akizungumza na masheha wa Mkoa wa Kusini Pemba mjini Chakechake, Ofisa Mratibu Elimu kutoka Tawala za Mikoa Zanzibar, Mkasi Hassan Thabit, alisema, ili kupunguza vitendo vya ukatili na udhalilishaji kwa watoto ni vyema masheha kuzibeba kesi hizo.

Alisema kuwa, iwapo masheha watasimamia na kuzibeba kesi za udhalilishaji wa watoto kwa kuzifikisha polisi na kuzifuatilia hadi mwisho, rushwa haitotokea, jambo ambalo litasaidia kupunguza ama kuondosha kabisa udhalilishaji.

"Tuwe na kawaida ya kuzibeba hizi kesi, tuzifuatilie kuanzia mwanzo hadi mwisho, kwa sababu kama kuna rushwa inatendeka nyinyi hamtodaiwa, wanaodai rushwa wataogopa," alisema ofisa huyo.

Aidha, alisema kufuatia janga la ugonjwa wa corona lililokuwa limeikumba nchi siku za nyuma, kumeibuka utoro wa wanafunzi, jambo ambalo linaweza kuwakosesha haki yao ya kupata elimu.

"Mtoto ana haki ya kulindwa dhidi ya majanga mbalimbali, lakini ana haki ya kupata elimu, hivyo tujitahidi kuhakikisha wanakwenda shule kama kawaida," alieleza.

Kwa upande wake Amiri Mdoe Amiri kutoka Tawala za Mikoa, alisema kuwa kuna haja kwa masheha kujipanga katika kuhakikisha wanapita nyumba kwa nyumba, kuwasaka watoto wasiokwenda shule na kuwapeleka.

"Tuhakikishe kwamba watoto wote hawabaki nyumbani wakati wa kwenda shule, tupite nyumba kwa nyumba kukagua na ikiwa kuna mzazi anachangia kutokwenda mtoto wake shule, achukuliwe hatua za kisheria," alieleza.

Alizitaka kamati za shule zifanye kazi kwa moyo mkunjufu, ili kuleta maendeleo kwao, wanafunzi, jamii na taifa kwa ujumla.

Akiwasilisha mada namna ya kumlinda mtoto, Ofisa Uratibu Tawala za Mikoa, Said Mohamed Said, alifahamisha kuwa, mtoto anahitaji ulinzi juu ya majanga mbalimbali yaliyomo ndani ya jamii, jambo ambalo litasaidia kupata taifa bora la baadaye.

"Tuwalinde watoto wetu juu ya magonjwa mbalimbali, udhalilishaji na pia majanga mengine yanayoweza kuwadhuru, tutapata watoto imara," alisema.

Suleiman Nassor Suleima, Katibu Shehia ya Mgogoni Wilaya ya Chakechake, alieleza kuwa utoro wa wanafunzi upo tangu kumalizika ugonjwa wa corona, ambapo shule yao ina wanafunzi watoro 64.

Naye sheha wa Shehia ya Mchangamrima, Omar Suleiman, aliishukuru wizara hiyo kwa kuwaamsha na kusema kuwa, watajitahidi kuzifuatilia shule, kuhakikisha kunakuwa na maendeleo mazuri ya wanafunzi na kamwe hawakumbwi na udhalilishaji pamoja na magonjwa mbalimbali.

# Asasi yaasa vitendo vya kuvunja amani

**Na Sabato Kasika**

WATANZANIA wametakiwa kuepuka kujiingiza katika vitendo ambavyo vinaweza kuvuruga amani, utulivu, umoja na mshikamano, badala yake wavilinde kwa manufaa ya vizazi vilivyopo na vijavyo.

Wito huo uliotolewa jana, jijini Dar es Salaam na Umoja wa Wanaharakati Wazalendo na Siasa Tanzania (UWAST), katika tamko lake kuhusu uchaguzi mkuu uliofanyika wiki iliyopita.

Kiongozi wa UWAST, Kunje Ngombale Mwiru, ndiye aliyesema hayo kwa waandishi wa habari na kusema baada ya uchaguzi kuna maisha, hivyo ni muhimu kila Mtanzania kuepuka vurugu na maandamano.

"Mambo ya msingi ambayo kila Mtanzania anatakiwa kuyapa kipaumbele ni kulinda amani, utulivu, umoja na mshikamano, kwa manufaa ya vizazi vilivyopo na vijavyo," alisema Kunje.

Alisema, umoja huo umetafakari kwa kina baada ya kuwapo kwa taarifa za baadhi ya vyama kutaka kuandamana kupinga uchaguzi mkuu, jambo ambalo amedai si sahihi na linatakiwa kupingwa.

"Sisi tunaamini kwamba uchaguzi ulikuwa huru na haki na tunashauri wale wanaohamasisha maandamano waache, wasubiri baada ya miaka waingie tena ulingoni kuliko kuleta vurugu," alisema.

Naye mwanachama wa umoja huo, Amina Ahungu, aliwataka Watanzania waendelee kushirikiana kujiletea maendeleo bila kujali itikadi za vyama vyao, kwa vile maendeleo hayana chama.

"Tunaunganishwa na Utanzania wetu, hivyo tuepuke mbinu zozote zenye lengo la kutugawa kwa itikadi za vyama ama kuhasimiana, bali tuendelee kuwa wamoja ili kuenzi amani yetu," alisema Amina.

Amina alisema, kampeni hadi uchaguzi mkuu vimefanyika kwa amani, hivyo kila Mtanzania aendelee kulinda akitambua kwamba ni lazima maisha yaendelee baada ya uchaguzi.

Aliwataka vijana kutokubali kuingizwa kwenye mtego wa kushiriki maandamano, badala yake wawakatae wanasiasa wenye nia ya kutaka madaraka kwa njia zisizo halali.



Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya TPB, Moses Manyatta (kulia), akizungumza kwenye hafla ya mkutano wakati wa ziara fupi ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera na Uwekezaji, Angela Kairuki (kushoto), aliyoifanya mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Waomba bei nzuri majani ya karafuu

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

WANANCHI wa Shehia ya Mgelema wameiomba kampuni ya kusindika majani makavu ya karafuu, kuwaongezea bei ya majani hayo, kutokana na kuwa bei iliyopo haikidhi mahitaji yao.

Walisema kuwa, kutokana na changamoto za kiuchumi wanazokabiliana nazo na ugumu wa kuyatafuta majani hayo, kuna haja kwa kampuni hiyo kuwaongezea bei, ili wapate hamasa ya kutafuta zaidi, jambo ambalo litasaidia kupunguza umaskini.

Walisema, bei iliyokuwa kununulia majani hayo ni ndogo sana kiasi kwamba inawarudisha nyuma katika kuendelea na kazi hiyo.

Walisema wameona faraja kuwapo kwa kiwanda hicho, ingawa watakapoongezewa bei watafurahi sana kwani watapata kipato kitakachowasaidia kupunguza ukali wa maisha.

Nachia Saleh Hamad alisema kampuni hiyo inanunua majani ya mkarafuu kilo Sh. 150, hali ambayo inawarudisha nyuma.

"Tunataka tuongezewe angalau kilo Sh. 500 kwani ni vigumu siku hizi kupata majani, kutokana na kuwa baadhi ya wamiliki wa mashamba hawataki, wanasema ni mbolea ya mikarafuu yao, hivyo hutufukuza na kututolea maneno," alisema.

Alisema kwamba kiwanda hicho ni chachu ya maendeleo kwao na vizazi vijavyo kwa kuendelea kujipatia kipato kitakachowawezesha kiuchumi.

Laila Zubeir Mdoe alisema kwa sasa upatikanaji wa majani hayo ni shida kutokana na kipindi chenyewe kilichopo kuwa hakuna zao la karafuu na pia shehia nzima wanategemea majani hayo.

"Shehia nzima tunategemea majani hayo kwa sababu hatuna kazi nyingine ya kutupatia pesa, hivyo yamekuwa ni machache, kwani kila kaya hutoka kwenda kutafuta," alieleza.

Naye Asha Mohamed Juma, alisema katika shehia yao wanawake hawakuwa na shughuli zozote za kufanya, kazi inayoweza kuwaingizia kipato, lakini baada ya kujengwa kiwanda hicho wanatafuta majani ya mkarafuu na kuuzia kampuni.

"Mwenyezi Mungu kazidi kuionyesha njia serikali yetu kwa kutuletea maendeleo kwa kuona kwamba, ipo haja ya sisi kutupatia chanzo cha kuwakomboa," alisema.

Ameir Said Mohamed alisema kutokana na changamoto wanazokumbana nazo katika utafutaji wa majani hayo, ameiomba kampuni hiyo ikawaongezea bei itakayowakomboa kiuchumi.

Nipashe
# TESA
Jumanne Novemba 3, 2020
TEKNOLOJIA · ELIMU · SAYANSI



Ukurasa 12

**Wanamageuzi wamekwama kufuta cheti, wangoje baadaye?**



Ukurasa 13

Watoto wanapokimbia darasa na kujitumbukiza baharini



Ukurasa 14

**Ahadi wapigakura wanasubiri maboresho makubwa elimu**

TEKNOLOJIA

**NA FAUSTINE FELICIANE**

# 'KWIKWI' ZA GMO

## ■Ni mbegu mfu hazipandwi mara 2
## ■Huleta utumwa na utegemezi

KILIMO kinatajwa kuwa ni kazi iliyokuwapo baada ya kuumbwa ulimwengu, ukulima unaelezwa kuwa ulianzia kwenye bustani ya Edeni.

Kwa hiyo, dhana kuwa ni shughuli ya karne nyingi na kongwe inawatafakarisha wataalamu kukiboresha kilimo kuanzia kutumia pembejeo mbalimbali kama mbegu za asili na zilizoboreshwa (chotara) zinazozalishwa katika vituo vya utafiti vya kilimo ndani na nje ya nchi.

Aidha, dhana hiyo inaibua masuala kama viuatilifu pamoja na jitihada za kutumia kemikali kuhifadhi chakula zinazofanyika kwa sababu kilimo kina umuhimu pamoja na mchango mkubwa kwenye maendeleo kuanzia kufikia lengo la kuwa na uhakika na usalama wa chakula, pembejeo za viwandani na ulinzi wa mazingira.



Wakulima wakichuja kiuatilifu cha asili mbadala wa dawa za sumu za kuulia wadudu za viwandani. **PICHA: TABIO.**

Hata hivyo, wakulima wanakabiliwa na changamoto zinazorotesha juhudi zao ikiwamo ukosefu wa mbegu bora, mabadiliko ya tabia nchi yanayoambatana na ukame, visumbufu pamoja na magonjwa.

Ili kukabiliana na changamoto hizo kumekuwa na ushawishi wa wadau kutoka ndani na nje ya nchi wa kuweka mazingira bora ya kuruhusu matumizi ya mbegu zinazotokana na teknolojia ya uhandisi jeni au 'Genetic Engineering' zinazozalisha mazao yaliyobadilishwa vinasaba -GMOs.

Wapo wanaokubaliana na ukweli kuwa hakuna sababu ya kubadilishi jeni za mazao, miongoni ni Bakari Mongo, Mkurugenzi wa Taasisi inayoendesha shughuli za kilimo hai nchini (TOAM).

Mongo akizungumza na Nipashe kuhusu kilimo hai na cha mazao ya GMOs, anafafanua kuhusu mimea ya GMOs.

Anaeleza kuwa viumbe au mimea iliyobadilishwa vinasaba ni ile ambayo imezalishwa kwa teknolojia ya uhandisi jeni au genetic engineering, inayohusisha kutenganisha kinasaba kinachojulikana tabia yake kutoka katika chembe hai ya kiumbe kimoja na kuhamishia nakala ya kinasaba hicho katika chembe hai ya kiumbe kingine, ili kuingiza tabia zinazohitajiwa hasa zilizobora.

Kwa mfano, Mongo anasema, kinasaba cha bakteria anayeishi kwenye udongo aitwaye bacillus thuringiensis (Bt), huyo anaishi ardhini na ana uwezo wa kutoa sumu ya kuangamiza baadhi ya wadudu.

Mtaalamu huyu anasema Bt anayeishi kwenye udongo ana sifa ya kutoa sumu (Bt toxins) ya kuua visumbufu vinavyobungua shina la mmea na hivyo kudhibiti uharibifu.

Hata hivyo, sumu yake haiwadhuru binadamu ndiyo maana anatumiwa kwenye jitihada hizo, kwa mujibu wa maelezo yake.

Kwa kutumia uhandisi jeni bakteria hiyo huhamishiwa kwenye mimea ili itoe sumu ya kuua wadudu wanaoibungua (stem borer). "Uhamishaji ukikamilika chembe hai iliyoingiziwa kinasaba kipya hukuzwa kwenye maabara mpaka kuwa mmea kamili." Anaeleza Mkurugenzi wa TOAM.

Zipo aina kadhaa za mimea iliyobadilishwa vinasaba tangu utafiti wa kuboresha mimea kwa kutumia teknolojia ya uhandisi jeni ianze mwanzoni mwa miaka ya 1980, anakumbusha.

Anaitaja kuwa ni mimea iliyobadilishwa vinasaba kwa kuingiziwa Bacillus thuringiensis ni pamoja na pamba na mahindi.

Anasema mimea inayovumilia sumu ya kuua magugu inazalishwa kwa kuingiziwa kinasaba kinachovumilia sumu ya kuua magugu yenye kiambato cha glyphosate.

Upuliziaji wa sumu hii kwenye mimea huua magugu yote bila kuathiri mimea husika. Mifano ya mimea hii ni mahindi, maharage ya soya, canola (sukuma wiki) na pamba.

"Mimea iliyobadilishwa vinasaba ili kutoa sumu ya kuua visumbufu vya mimea na ukinzani dhidi ya kemikali za kuua magugu na visumbufu vya mimea (Bt toxins), wakati huo huo, ikiwa na uwezo wa kuhimili sumu ya round up inayopuliziwa shambani kuua magugu," anasema Mongo.

**KUONGEZA VIRUTUBISHO**

Jitihada za kuimarisha afya ya binadamu kwa mimea iliyobadilishwa vinasaba ili kuongeza virutubisho ni kazi iliyofanyika barani Asia, mpunga ukiingiziwa kinasaba cha kutoa kirutubisho cha vitamin A na kupewa jina la mpunga wa dhahabu (golden rice), anasema Mkurugenzi wa TOAM.

Lengo kuu likiwa ni kukabiliana na upungufu wa vitamini hiyo hasa kwa watoto wadogo.

**CHANGAMOTO**

Mongo akizungumzia changamoto zinazotokana na mimea iliyobadilishwa jeni anasema ni pamoja na umiliki wa mfumo wa chakula, kwani teknolojia ya uhandisi jeni inahusisha utaalamu wa kuzuia mbegu za mimea hiyo kuota na kuzaa tena pale zinapopandwa mara ya pili.

Aidha, inazikwamisha kutoa mazao mazuri ukilinganisha na yale ya awali. Teknolojia hii humwongezea gharama mkulima mdogo kwa kumlazimisha kununua mbegu kila msimu, anasema.

Kwa mujibu wa maelezo yake wakulima pia wanalazimika kwa kiasi kikubwa kununua mbolea na viuatilifu kutoka kwa kampuni inayowauzia mbegu hizo.

Aidha, hupunguza wigo wa kibiashara, kukwamisha kupata masoko mengi kwa mfano mataifa ya Umoja wa Ulaya (EU), hayaruhusu uingizwaji wa mazao yaliyobadilishwa vinasaba kwa matumizi ya binadamu.

Anasema kinasaba cha bakteria Bacillus thuringiensis (Bt) kinapoingizwa katika mazao ya pamba na mahindi hutoa sumu inayoua viwavi waharibifu wa mazao hayo.

Sumu ya Bt huzalishwa katika

**INAENDELEA UK.12**

ELIMU

NA MICHAEL ENEZA

# Wanamageuzi wamekwama kufuta cheti, wangoje baadaye?

WIKI chache zilizopita yalisikika matangazo ya mabadiliko ya mfumo wa mafunzo ya ualimu ikitangazwa rasmi kuanza kwa mfumo ambao utaondoa mafunzo ya ualimu wa ngazi ya cheti na kubadilisha walimu waliopo wa ngazi hiyo, wakiambiwa hawana budi kujiendeleze na pia

wastaafu kwa awamu.

Hapakuwa na dhamira ya kumwondoa kazini mwalimu yeyote wa ngazi ya cheti, lakini hata suala la kuhitajiwa kujiendeleza kupata 'stashahada' lilikwama.

Ni baada ya kulitupia macho suala hilo, Rais John Magufuli, akiwashangaa wapanga mitaala wizarani kwa kutoa pendekezo na kuanza kulitekeleza kufuta ngazi ya cheti katika utumishi wizarani.

Akitoa salamu kwa kongamano la fani ya ualimu lililokuwa linaendelea wakati huo, katika kipindi ambacho kampeni za uchaguzi mkuu zilikuwa zinaendelea, Rais Magufuli aliwaelekeza walimu kupuuza tangazo hilo, kuwa halina mantiki.

Alieleza hisia zake za kuheshimu ualimu ngazi ya cheti, hakuona haja ya kuwataka walimu wa ngazi hiyo kujiendeleza, ili kwenda na wakati kitaaluma.

Yako mapana na marefu ambayo ni wazi yalishapitia mijadala ya kitaaluma na upande wa mageuzi ndiyo ukashinda, kuwa ipo haja ya walimu kujiendeleza endapo waliishia ngazi ya cheti katika mafunzo ya kufikia ajira wizarani, au kwenye ofisi za Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI).

Ndiyo hapo lilipo tatizo, kama kuna haja ya kubadilisha mitaala kuondoa ualimu ngazi ya cheti au iwapo ngazi hiyo inahitaji kutambuliwa kama taaluma isiyo na doa, hivyo kuibakiza katika mafunzo ya ualimu na siyo ngazi ya kufikia taaluma halisi kama mabadiliko yanayotafsiri.



Wanafunzi wa darasa la awali wakifurahia baada ya kuhitimu. **PICHA: MTANDAO.**

Swali linabaki ualimu ngazi ya cheti ni taaluma tosha au ni ngazi tu ya kupandia?

Wanamageuzi wizarani wanaamini kuwa ngazi hiyo ni hatua ambayo baadhi ya walimu walipitia na kupata ajira, lakini kwa sasa haitoshi, kwani weledi unahitajiwa katika kufundisha.

Hivi sasa kuna ngazi tatu ambazo wataalamu wizarani wanaona ndiyo ziendelezwe nazo ni 'astashahada,' 'stashahada' na 'shahada' yenyewe, 'istilahi' hizo zikiwa zimeundwa ili kukwepa maneno rahisi tu ya cheti, diploma na digrii.

Hiyo 'astashahada' na 'stashahada' zinakaribiana kwani vyuo vingi vinatoa diploma ya kawaida kwa miaka miwili ya masomo halafu diploma ya juu (advanced diploma) kwa mwaka mwingine mmoja, iwe ni katika fani za uhasibu au kwingineko.

Ualimu mfumo wake ulikuwa ni cheti (certificate) kwa yule aliyemaliza kidato cha nne, halafu diploma kwa aliyemaliza kidato cha sita na digrii (shahada) kwa wale waliomaliza vyuo vikuu, hivyo ngazi ya 'astashahada' na 'stashahada' ingehitaji 'cheti' kiwe ni wale zamani waliitwa 'ngumbaru,' waliofyatuliwa kutoka darasa la saba kujazia mapengo ya kuandikisha wanafunzi wengi, lakini haielekei kuwa bado wako TAMISEMI. Hao wa vyeti zaidi ni wa kidato cha nne.

Lipo suala la msingi ambalo wataalamu wizarani wanajaribu kutoa majibu mapya kuhusu nini kifanyike, kuhusu ufundishaji katika shule za msingi na hasa za awali halafu darasa la nne.

Hivi kuna haja ya walimu wa 'astashahada' na 'stashahada' katika ngazi hiyo au wale wa 'cheti' wanatosha? Jibu la mgombea urais wa CCM lilikuwa moja kwa moja kuwa cheti kinatosha kwa ngazi hiyo na kibaki hivyo, isionekane kuwa kufundisha watoto wa ngazi hiyo ni hatua tu ya kupanda ngazi kufundisha wale wa madarasa ya juu zaidi.

Na kimsingi yuko sahihi kuna wito maalum wa kufundisha watoto, si ngazi kama mabadiliko yaliyoandaliwa wizarani yanavyoashiria, kuwa unajilazimisha kufundisha madarasa hayo ya chini, barua zijazwe TAMISEMI za kuulizia kupanda ngazi (au cheo) na pia kubadilishiwa hayo madarasa.

Kwa maana hiyo ufundishaji watoto wadogo zaidi unakosa mwenyewe. Baadhi ya wale waliosoma zamani tena katika vijiji ambavyo elimu iliingia mapema wanaweza kuwa na kumbukumbu ya walimu waliokuwa wanafundisha darasa la kwanza na la pili wakabaki hivyo kwa vizazi viwili.

Walikuwa ni walimu wanaokumbukwa na kuenziwa na kila mwanakijiji hasa aliyepeleka mwanawe au aliyesoma shule hizo na walikuwa wanafahamu saikolojia ya watoto kama wanavyofahamu viganja vyao.

Licha ya kuwa siyo wengi kati ya walimu hasa hawa wa kizazi cha 'dot.com' wanaoweza hata kuwaza kufikia rekodi hiyo, unaweza kuona waziwazi kuwa kufundisha watoto wadogo ni taaluma halisi, ambayo inahitaji zaidi kuboreshwa.

Mwalimu wa ngazi ya cheti ni mlezi wa aina fulani na mwalimu kwa upande mwingine au ni baba mdogo kwa njia moja au nyingine halafu anakuwa mwalimu.

Siyo kila mwalimu apachikwe afundishe madarasa hayo, abwabwaje peke yake hajui watoto wana uelewa wa kasi kiasi gani na wanahitaji vielelezo gani.

Ndiyo hapo watoto wanafika darasa la saba hawajui kusoma na kuandika kwani wahitimu wa 'astashahada' na 'stashahada' wanapigania kuinuliwa madarasa wanapuuza watoto.

---

INATOKA UK.11

# 'KWIKWI' ZA GMO

mmea wakati wote mmea unapokuwa na hivyo kuwafanya baadhi ya wadudu kuizoea na kujijengea usugu.

**MADHARA WASIOKUSUDIWA**

Mratibu wa Tasisi ya Kilimo Tanzania (TABIO), Abdallah Mkindi, akizungumzia madhara kwa wadudu wasiokusudiwa yanayotokana na sumu ya Bt toxins inayotolewa na mmea uliobadilishwa vinasaba, anasema inakuwa tayari kushambulia wakati wote na hali hii husababisha baadhi ya wadudu rafiki wa mazingira kuuawa.

MAGUGU SUGU

Mtaalamu huyu anasema magugu kujijengea usugu dhidi ya viuadudu ni changamoto nyingine, kwa hiyo mazao yaliyobadilishwa vinasaba yanazalishwa kustahimili sumu za magugu za aina ya glyphosate na glufosinate.

Hii ikimaanisha kuwa sumu hizo huua magugu yote shambani na kubakiza mazao yaliyokusudiwa tu.

Hata hivyo, magugu sugu yameshajitokeza na kuongeza matumizi zaidi ya viuatilifu vyenye kuleta madhara kwa binadamu na viumbe wengine.

**MAZAO HAYAISHI PAMOJA**

Mazao yaliyobadilishwa vinasaba hayawezi kuishi pamoja kwa kitaalamu 'co-existence' na yale ya asili bila kuyachafua.

Mimea inayotokana na mbegu zilizobadilishwa vinasaba huchafua yale ya asili na hatimaye mbegu hizo kupotea.

Wakulima wanaweza kushtaki mahakamani na kudai kulipa mrahaba ikiwa mazao yao yatakutwa yana viini vya mazao yaliyobadilishwa jeni kwa zaidi ya asilimia tisa.

Mazao yaliyobadilishwa vinasaba yamewekewa haki miliki ya kitaaluma ambayo humzuia mkulima kuyahifadhi kwa matumizi ya msimu ujao wa kilimo, hivyo kulazimika kununua mbegu kila msimu unapowadia.

Mazao yaliyobadilishwa vinasaba hutishia uwepo wa mazao ya kilimo hai hivyo ni adui wa kilimo endelevu.

"Wakulima wengi wanatumia mbinu za kilimo endelevu na kilimo hai katika uzalishaji mazao. Kuruhusu matumizi ya mbegu zilizo badilishwa jeni huingilia na kuharibu mfumo wa kilimo na masoko ya bidhaa za kilimo hai," anasema Mkindi.

Aidha ni chanzo cha mmomonyoko wa vinasaba kwani matumizi ya mbegu zilizobadilishwa vinasaba huchafua mfumo wa kijenetiki wa mbegu za asili, anaongeza.

Anaulezea uchafuzi huo kuwa huchangia kumomonyoa vinasaba kwa kuwa haiwezekani kuyarudisha katika sifa na hali yake ya asili.

**CHA KUFANYA**

Swali kubwa linalowatafakarisha wakulima wa kilimo hai ni hili ni nini kifanyike ili kukabiliana na mbegu zilizo badilishwa jeni?

Mkindia anasema mosi ni kuhamasisha serikali, ili kusimamia kwa ukamilifu sheria ya matumizi salama ya mazao yaliyobadilishwa vinasaba.

Jingine ni kutoa elimu kwa wakulima na wadau wengine kuhusu mbegu zilizobadilishwa vinasaba.

" Kuishawishi serikali iendelee kubakiza kipengele cha 'strict liability' kinachoelezea uwajibikaji kwa watakaoingiza mazao yaliyobadilishwa vinasaba hasa kwa wakulima na walaji pindi yanapotokea madhara," anasisitiza.

Mratibu wa TABIO anasema jukumu jingine ni kufanya kazi na vikundi vya wakulima ili kuimarisha mifumo ya ubadilishanaji wa mbegu za asili na kukubali au kuchukua kauli ya anuai za mbegu na kanda huru za mazao yaliyobadilishwa jeni (GMO free zones).

Anasema kingine ni kufuatilia taarifa za bidhaa zenye GMOs katika mnyororo wa chakula (food chain) ili ziondolewe.

Anasisitiza kutembeleana kati ya jamii zenye anuai nyingi za mbegu na zile kanda huru za mazao yaliyobadilishwa jeni.

"Jingine ni kufanya kazi kwa kushirikiana na vyuo vya utafiti vya kilimo ili kuzalisha mbegu bora za asili." Anasema Mratibu wa TABIO.

ELIMU

NA BEATRICE PHILEMON

# Watoto wanapokimbia darasa na kujitumbukiza baharini

UKIANGALIA juhudi za serikali za kugharimia elimu kuanzia shule ya msingi hadi sekondari na ukichunguza kinachofanywa na baadhi ya wazazi na walezi katika Kijiji cha Mdimni kilichopo, wilayani Mkuranga Mkoa wa Pwani, kuna mengi ya kushangaza.

Wazazi na walezi, hawana hamasa ya kusaidia watoto wao kielimu badala yake huwaelekeza baharini kuvua uduvi au dagaa kamba, anasema Said Msati, mjumbe wa serikali ya kijiji hicho.

Akizungumza na Nipashe, mwanakijiji huyo, anasema watoto wengi wa kike na kiume kuanzia miaka 12-18 wanatumia muda mwingi kuvua, ili kujipatia fedha kwa ajili ya kujisomesha, mavazi, chakula, tiba kwa sababu wazazi wengi hawana kitu.

"Watoto wanakwenda kwenye mikoko kuvua kamba wadogo maarufu kama uduvi kujiongezea kipato, kwa kuwa asilimia 80 ya wakazi wa kijiji cha Mdimni wanategemea uvuvi na biashara pamoja na huduma nyingine za kijamii baada ya nazi kukauka."

"Wazazi wengi wamekuwa maskini kwa sababu awali walitegemea minazi kwa ajili ya kujiongezea kipato, lakini kwa jua lililopiga miaka 15 iliyopita kuanzia 1999 hadi 2006, minazi yote asilimia 60 imekufa, imekauka na jamii hivi sasa inategemea shughuli za uvuvi, ukataji wa mkaa pamoja na kilimo chetu cha jembe la mkono," anasema Msati.

Ingawa walimu wamekuwa wakifanya jitihada mbalimbali kufundisha wanafunzi, wazazi katika kijiji hiki wanawaangusha kwa sababu watoto hawapati muda wa kujisomea, wakati wote wanautumia katika kazi za nyumbani na biashara za kusaka pesa."

"Kwa mfano mtoto wa kike akirudi nyumbani anatumwa kuvua samaki, akitoka huko anakwenda kisimani, kisha kuni, kutwanga kisamvu au muhogo kwa ajili ya ugali, lakini apike chakula anakamatwa mpaka saa 3:00 usiku," anasema Msati.

Anaongeza kuwa kwa muda huo anakuwa amechoka hawezi tena hata kusoma matokeo yake anaamua kulala mpaka asubuhi akienda shuleni anarudi na ratiba ni hiyo," anasema.

**MAMIA NI MBUMBUMBU**

Kutokana na changamoto hiyo: "Hivi sasa tuna takribani vijana 150 waliomaliza elimu ya sekondari katika Shule ya Magawa ambao hawajui kusoma," anasema Msati.

Sekondari Magawa ni shule ya kata ambayo inatumiwa na vijiji vitano vya Magawa, Mdimni, Ng'anje, Kengeni na Makumbeya.

Pia, hata mtoto akiwa anapenda kusoma mzazi au mlezi anamkatisha tamaa, anamwambia ajifelishe kwenye masomo na anapofaulu analaumiwa kwa nini amefaulu.

"Hii ni tabia inayokwamisha ndoto za watoto, wewe kama mzazi inabidi umpongeze mtoto ili aweze kuongeza bidii zaidi, lakini cha kushangaza katika kijiji chetu mzazi au mlezi anakasirika na kusema mtoto kwa kazi nzuri hadi kufaulu." Anasema Msati.

Ili kusaidia wananchi kujua umuhimu wa elimu ni vizuri wadau wa elimu au maofisa elimu watembelee katika wananchi na kuhamasisha umuhimu wa elimu kupitia mkutano mkuu wa kijiji, anasema.

Anaeleza kuwa wazazi wanaweza kubadilika na kusaidia watoto wao kupenda elimu ambayo itasaidia kuleta maendeleo katika familia zao na kuondokana au kupunguza umaskini.

**ATOA USHUHUDA**

"Nilioa mke wangu mwaka 2004 nilimkuta na mtoto mwenye miaka mitano. Ni baada ya kuachwa na mumewe na pia hakuwa na huduma yoyote ya kumtunza mtoto huyo." Anakumbusha Msati.

Anaeleza kuwa alipofikia umri wa kwenda shule alimpeleka shuleni akasoma kuanzia darasa la kwanza hadi la saba na akafaulu.

"Baada ya mtoto kufaulu, baba mdogo na mke wangu alinifuatilia nyumbani na kuanza kunifokea, kwa nini umemwambia mwanao afanye vizuri darasani? Mbona unajipendekeza kwetu sisi ili mtoto afaulu vizuri, wewe una uwezo gani wa kumsomesha achana naye kabisa aliongea kwa jaziba sana anasema," anakumbusha.

Anasema alimsikiliza kwa makini huku akimshangaa, baadaye aliamua kumwacha yule mzee kama alivyo na alivyoondoka yeye na mke wake walijitahidi kumsomesha mtoto huyu kwa siri hadi kidato cha nne.

"Sasa hivi nimeanza kuona mafanikio ya mtoto niliyemsomesha Mungu amemsaidia amepata kazi yuko Kariakoo na amekuwa mkombozi katika familia yangu na na ya baba mkwe wangu aliyenikataza kumsomesha ndiye anayemtegemea." Anasema.

Mbali na hilo kila sikukuu huyu mtoto ndiye anayewanunulia ndugu zake wawili mavazi, chakula na hugharamia pesa hata Sh. 100,000 kufanikisha sikukuu," anasema.

Mbali na hilo pia anawaachia hela za matumizi, pia mama yake na yeye mlezi wake anajitahidi kuwatumia wastani wa Sh. 15,000 kila wiki.

"Ingawa mke wangu ni mlemavu hasikii lakini niliweza kuongea naye akanielewa na hatimaye tukaweza kumsomesha mtoto wetu," anasema Msati.

Mbali na hilo, nimekuwa nikiwafundisha watoto wangu wawili kwa muda wa miaka mitano kutoka wakiwa wadogo jinsi ya kuongea na mama yao kwa lugha ya ishara, hivi sasa wanangu wanaweza kuongea na mama yao bila matatizo.

"Niliamua kufundisha watoto wangu lugha ya ishara, ili isiwe changamoto kwao wakitaka kumwambia mama vitu wanavyohitaji, matatizo au changamoto zinazowakabili kama mimi sipo," anasema.

**WALIMU WATUHUMIWA**

Akizungumzia suala hilo, Mwenyekiti wa Kijiji, Adam Ulanga, anakanusha kuwa watoto hawajitumi kusoma na wazazi kuwakwamisha.

"Watoto wanajitahidi sana kusoma wakiwa shule ya msingi ila kuna baadhi ya walimu hawajitumii kufundisha watoto wetu."

Anasema Kijiji cha Mdimni kilichoanzishwa mwaka 1971, hadi kina wakazi 1,332 na kaya maskini 90 na hakina umeme.

Ulanga anawatetea watoto kuwa wanakwenda shule, lakini kuna baadhi ya walimu hata madarasani hawakai wanakuja shule mara mbili na hata wakifika hawafundishi.

"Unategemea mtoto atawezaje kuendelea vizuri katika masomo yake," anahoji.

Anasema mwaka 2019, Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga ilileta walimu watatu shule ya Magawa, lakini walimu hawa hawakai shuleni.

Wanafanya kazi Jumatano na Alhamisi siku nyingine hawaonekani na ikifika Ijumaa wanaondoka. Akizungumzia mazingira ya shule, alisema yamechakaa na kuomba uongozi wa Wilaya ya Mkuranga na wadau wengine wawasaidie kukarabati madarasa na nyumba za walimu kwani hali hairidhishi.

"Miundombinu ya shule siyo mizuri, sakafu za madarasa ni chakavu, nyumba za walimu tatu pia chakavu kwa hiyo walimu wanafanya kazi, ili mradi tu maisha yaende, tunaomba halmashauri itusaidie kuboresha shule yetu ili wanafunzi waweze kusoma katika mazingira mazuri," anasema.

**DC HAJAFAHAMISHWA**

Mkuu wa Wilaya ya Mkuranga, Filberto Sanga, anapoulizwa anajibu: "Nashukuru kupata taarifa hii nitakwenda wiki ijayo kukutana na wananchi ili kujua changamoto zao,"

"Shule ya Msingi Magawa ni ya kijiji kwa hiyo wanakijiji wanawajibika washirikiane na serikali kujenga nyumba za walimu, ili watoto wasome vizuri, walimu waweze kufundisha katika mazingira bora na na pia kuishi mahali salama," anasema.

Akizungumzia walimu kushindwa kukaa shule, anahoji jamii ya eneo inawapa walimu ushirikiano. Mkuu wa shule yuko karibu na walimu kufanya nao kazi na kijiji ndicho kinatakiwa kisimamie kujenga nyumba za walimu, halafu serikali inaongeza nguvu, wanafanya hivyo?




Wanafunzi wanahitaji mazingira bora ya kufundishwa na walimu ya kufundishia, ili kuendeleza elimu bora. Wazazi kushirikiana na walimu na watoto wao ni muhimu ili wafikie elimu bora. **PICHA: MTANDAO**

SAYANSI

NA SABATO KASIKA

# Ahadi wapigakura wanasubiri maboresho makubwa ya elimu



Katibu wa Itikadi na Uenezi wa CCM, Humphrey Polepole, akionyesha Ilani ya uchaguzi ya chama ya mwaka 2020/2025. **PICHA: MTANDAO**

MAFUNZO ya ufundi stadi ni nyenzo muhimu inayoweza kumsaidia mwanafunzi kujiajiri mara anapohitimu na kumwezesha kujiletea maendeleo, badala ya kusubiri kuajiriwa.

Kwa kutambua hilo, katika ilani ya uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020- 2021, inaahidi katika kipindi cha miaka mitano ijayo, kitahimiza serikali kuimarisha utoaji wa elimu hiyo.

Ilani hiyo inasema, elimu itaimarika kwa kuwajengea uwezo wakufunzi na wahadhiri na kuvipatia vyuo vifaa vya kisasa, ili kuzalisha wataalamu wenye kukidhi mahitaji ya soko la ndani na nje ya nchi.

Pamoja na hayo jambo jingine ni kuhuisha mitaala na kuanzisha programu kulingana na mahitaji ya kitaifa, kikanda na kimataifa ambayo yanaendana na mapinduzi ya nne ya viwanda.

Aidha, kingine kinachokusudiwa kufanywa, ni kuongeza udahili wa wanafunzi wa elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi, kuimarisha udahili wa wanafunzi wa stashahada za ufundi kwa lengo na kuimarisha uwiano wa idadi za wahandisi, mafundi na mafundi mchundo ili kuongeza ufanisi katika sekta za ujenzi na uzalishaji viwandani.

Mengine yanayotarajiwa kufanywa na serikali ya CCM ni kuweka mazingira wezeshi kwa kujenga na kukarabati vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi, ili kuongeza idadi ya wahitimu.

Kuanzisha utaratibu wa kuwakopeshwa vifaa na mitaji kwa masharti nafuu wanafunzi wanaohitimu mafunzo ya ufundi, kujenga vyuo viwili vya elimu ya mafunzo ya ufundi vya ngazi ya kati ni mengine, ambayo hayakuachwa nyuma.

Kinachokusudiwa hapo ni kuongeza fursa za upatikanaji wa elimu ya ufundi na pia kuboresha utekelezaji wa utambuzi na urasimishaji wa ujuzi unaopatikana nje ya mfumo rasmi wa utoaji elimu.

AHADI NI DENI

Kwa ujumla kuna ahadi nyingi ambazo zimo katika ilani ya chama hicho kwa ajili ya kuboresha elimu nchini, ikiwamo elimu ya msingi hadi sekondari, ambayo itaendelea na mpango wa kutolewa bila malipo.

Lengo la kufanya hivyo, ni ili kuwezesha vijana wenye sifa kuendelea na masomo bila kikwazo, lakini kila shule ya msingi itakuwa inatoa elimu ya awali kwa ufanisi katika mazingira na miundombinu iliyoboreshwa, kuimarisha utoaji wa elimu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum.

Mkazo zaidi unakusudiwa kuwekwa katika kuimarisha ufundishaji wa masomo ya sayansi yakiwamo Hisabati, Fizikia, Kemia na Baiolojia na kuongeza upatikanaji wa walimu wa kufundisha masomo hayo.

Ujifunzaji na ufundishaji wa masomo ya stadi za kazi na lugha ikiwamo ya alama katika elimu ya msingi, vitaimarishwa, na pia uimarishaji wa masomo ya maadili, uzalendo wa kitaifa na uraia kwa shule zote nchini.

Hizo zote ni ahadi ambazo ziko katika ilani hiyo, ambazo Watanzania wanasubiri zitelekezwe kwa ajili ya kuendelea kuboresha elimu, hivyo ziishie kuandikwa tu bali zifanyiwe kazi.

Lakini ni vyema kukumbusha kuwa ahadi ni deni, hivyo ni wajibu wa walioahidi kuhakikisha kwamba wanatimiza, kwani tayari wameshapewa ridhaa na Watanzania kuongoza nchi kwa miaka mitano ijayo.

Ikumbuke kuwa katika kinyang'anyiro cha uchaguzi mkuu uliofanyika Oktoba 28, kila chama kilichoshiriki uchaguzi huo, kilikuwa na ilani yake yenye mikakati mbalimbali ya kuboresha huduma za jamii ikiwamo elimu.

Hata hivyo, CCM imefanikiwa kubaki madarakani, hivyo kinachotakiwa sasa ni kutimiza ahadi ambazo kimeahidi katika ilani yake ikiwamo ya uboreshaji wa elimu, ili kiendelee kuaminiwa na Watanzania.

MIAKA 5 ILIYOPITA

Chama hicho kinasema katika ilani yake kuwa serikali imeongeza uandikishaji katika elimu ya msingi kutoka wanafunzi 8,298,282 mwaka 2015 hadi kufikia wanafunzi 10,605,430 mwaka 2020.

Kinaongeza kuwa kumekuwapo na uboreshaji wa fursa za upatikanaji wa elimu, ambapo idadi ya madarasa imeongezeka kutoka 115,665 mwaka 2015 hadi kufikia 136,292 mwaka 2020 na kuongeza idadi ya shule za msingi kutoka 16,899 mwaka 2015 hadi 17,804 mwaka 2020.

Mafanikio mengine yanayotajwa ni kuongezeka kwa uwiano wa kitabu cha kiada kwa mwanafunzi wa darasa I-VI hadi kufikia wastani 1:2, na kwamba serikali imekuwa ikigharamia uchapishaji na usambazaji wa vitabu.

Aidha, kuongezeka kwa idadi ya wanafunzi wanaohitimu elimu ya msingi kutoka asilimia 67 mwaka 2015 hadi asilimia 81 mwaka 2020 na ufaulu wao kuongezeka kutoka asilimia 57 mwaka 2015 hadi asilimia 82 kwa mwaka 2020, vinatajwa na chama hicho kama sehemu ya mafanikio.

Vilevile, idadi ya wanafunzi wanaoendelea na kidato cha kwanza, inatajwa kuongezeka kutoka asilimia 56 mwaka 2015 hadi asilimia 86 mwaka 2019, huku uandikishaji wa wanafunzi katika elimu ya sekondari nao ukiongezeka.

Hao ni wa kidato cha kwanza hadi ya nne, kutoka 1,648,359 kwa mwaka 2015 hadi kufikia 2,185,037 mwaka 2019, na kidato cha nne hadi cha sita ni kutoka 126,024 kwa mwaka 2015 hadi kufikia 153,420 mwaka 2019.

Lakini CCM inajivunia ongezeko la fursa za upatikanaji wa elimu ya sekondari, kwa kuongeza idadi ya shule za sekondari kutoka 4,708 mwaka 2015 hadi kufikia shule 5,330 mwaka 2020.

MAFANIKIO ZAIDI

Kuna mafunzo mbalimbali ya jinsi ya kuanzisha vituo vya ubunifu kwa taasisi za elimu ya juu, ambayo yaliwezesha kuanzishwa kwa kambi za ubunifu katika vyuo vikuu vikiwamo Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Vyuo vingine ni Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo, Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela, Chuo Kikuu cha Dodoma, Chuo Kikuu cha Iringa na Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia.

Aidha, CCM inasema, imejenga maktaba ya kisasa katika Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 2,500 kwa wakati mmoja.

Mbali na hayo, wameibuliwa na kutambua wabunifu wachanga 415 kupitia mashindano ya kimataifa ya sayansi teknolojia na ubunifu ambao kati yao, wabunifu 60 mahiri wanaendelezwa ili wafikie hatua ya juu na hivyo kuongeza fursa za ajira kwa vijana.

Vilevile, vimeanzishwa vituo atamizi 17 vya kukuza na kuendeleza ubunifu na hivyo kuwezesha kuanzishwa kwa kampuni 94 zinazotokana na ubunifu.

Uwekwaji wa vifaa vya kompyuta yenye uwezo mkubwa (super computer) katika vituo vipya vya kuendeleza ubunifu na ujasiriamali katika fani ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) kwenye Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela Arusha na Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam, umefanyika.

Ilani hiyo pia inasema, miradi 139 ya utafiti, 47 ya ubunifu na mingine 29 ya kuboresha miundombinu ya maabara za utafiti katika Taasisi za Elimu ya Juu na utafiti, vimetekelezwa na pia watafiti 579 wamejengewa uwezo katika masomo ya ngazi ya umahiri na uzamivu.

# Wanaomaliza kidato cha 4 wapewa somo

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

WANAFUNZI wanaotarajiwa kuhitimu kidato cha nne mwaka huu, wametakiwa kujiepusha na makundi ya kihalifu yatakayozima ndoto zao kielimu.

Mkurugenzi wa Umoja wa wanafunzi Makanisa ya Kipentecoste Tanzania (CASFETA) Mkoa wa Dodoma, Mchungaji Hezron Sadick, aliyasema hayo jana alipokuwa akizungumza na wazazi na wahitimu hao kwenye mahafali yao yaliyofanyika Kanisa la TAG Sanctuarity Chadulu, jijini hapa.

Alisema wanafunzi hao wa kidato cha nne wanaotarajia kufanya mtihani wa kumaliza elimu hiyo Novemba mwaka huu wanatakiwa kutambua kuwa wao ni viongozi wa baadae hivyo wanapaswa kuwa waadilifu.

"Hakikisheni mnajiepusha na viashiria vyovyote ambavyo vinavyoweza kuzimisha ndoto za kujiendeleza zaidi kielimu," aliwaasa.

Alisema kuwa serikali inahitaji viongozi wasomi wasiojihusisha na usaliti juu ya nchi yao, wasiopokea na kutoa rushwa.

"Ni matumaini yetu mtasimama na Mungu kwa kujiepusha matendo maovu," alisema.

Kadhalika, aliwasisitiza wahitimu hao kujiepusha na utandawazi ambao unasababisha kuwa na mmomonyoko wa maadili na kushindwa kufikia malengo yao.

'Ili muweze kufikia haya yote kwanza mnatakiwa kusimama na Mungu, kusoma kwa bidii, kujiepusha na utandawazi ambao vijana wengi wamejikuta wakiharibika kutokana na kuchukua muda mrefu wa kuangalia," alisema.

Aidha, aliwaasa kutokuwa na maono ya kutaka kuolewa na kuoa kabla hawajafikia malengo ambayo yatawasaidia kujiletea maendeleo kwenye maisha yao.

"Msipange kuolewa na kuoa huku wakati elimu yenu haijafikia malengo, mnatakiwa kujiendeleza zaidi kielimu huku mkimtanguliza Mungu mbele ili mfanikiwe maisha yenu ya kila siku," alisema.

Kwa upande wake, Makamu Mkurugenzi wa umoja huo, Mwalimu Praise Samson, aliwataka kuiombea nchi pamoja viongozi ambao tayari wamechaguliwa ili watakapoanza kufanya kazi wafanye kwa kumtanguliza Mungu.

Alisema kuwa wahitimu hao ni sehemu ya Watanzania ambao pia wanajukumu la kuomba kwa ajili ya nchi na viongozi ambao tayari wamepewa jukumu la kulitumikia Taifa.

# Polisi Dodoma waimarisha ulinzi

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

JESHI la Polisi mkoani Dodoma limejipanga kuimarisha ulinzi na usalama kwa kufanya doria mbalimbali katika sherehe ya kuapishwa Rais mteule Dk. John Magufuli Novemba 5, mwaka huu.

Sambamba na hilo, limetoa onyo kali kwa watu wanaotaka kuandamana kupinga matokeo ya uchaguzi mkuu uliofanyika Oktoba 28, mwaka huu.

Akizungumza jana na waandishi wa habari jijini hapa, Kamanda wa Polisi mkoani humo, Gilles Muroto, alisema sherehe hiyo itafanyika katika Uwanja wa Jamhuri Dodoma na hali ya usalama kwa sasa ni shwari.

Alisema jeshi hilo litafanya doria mbalimbali za miguu, magari na kwa kutumia mbwa ili kuimarisha ulinzi wakati wote wa maandalizi na kuapishwa kwa rais huyo.

"Kwa ujumla Jiji la Dodoma lipo shwari kila mmoja anafanya shughuli zake za maendeleo, napenda kuwaambia wageni wote wanaotarajia kuja

katika shughuli za kuapishwa kwa Rais waje wakiwa na amani jeshi lipo na limeweka ulinzi katika kila eneo," alisema Muroto.

Alisema jeshi hilo lina nguvu ya kutosha na wanavikundi vya polisi jamii ambao wamefanyiwa mafunzo hivyo watalinda raia na mali zao.

Aliwataka wamiliki wa nyumba za kulala wageni na watoa huduma ya usafiri kutoa huduma inayostahili kwa wageni.

Kuhusu maandamano, Kamanda Muroto alisema jeshi hilo, limejipanga vizuri kila kona kwa

kuimarisha ulinzi katika maeneo mbalimbali na yeyote atakayethubutu kuandamana atakumbana na mkono wa sheria.

"Kitu kinachoitwa maandamano haramu hakitakiwi barabarani, mtu akiingia barabarani ina maana anataka kulichokoza Jeshi la Polisi

na tutawapiga kipigo cha mbwa koko maana kipigo cha mbwa kachoka wamepigwa kwenye sanduku la kura na wananchi," alisema.

Alibainisha kuwa kila mtu ameona katika uchaguzi uliopita aliyechaguliwa kapita kihalali, kwa hiyo hakuna sababu ya watu kujitokeza kufanya maandamano haramu ambayo hayakubaliki.

"Jeshi la Polisi limeelekezwa kufanya kazi chini ya kifungu cha tano sura 322 cha sheria ya polisi na polisi wasaidizi, ambapo kifungu hicho kimeeleza kazi za kufanya ni kupeleleza, kukamata, kufikisha watuhumiwa mahakamani, kulinda sheria na amri zinazotolewa na nchi au serikali na vyombo vya sheria lakini pamoja na hayo watabeba bunduki," alisema.

Kamanda huyo alisema polisi watahakikisha Watanzania wanalindwa kwa gharama yoyote ile

na hawatakubali watu wachache waharibu amani ya nchi ambayo ina watu zaidi ya milioni 55.



Askari wa vikosi mbalimbali vya Jeshi la Polisi mkoani Dodoma, wakifanya mazoezi ya utimamu ikiwa ni sehemu ya kujiweka sawa kukabiliana na wafuasi wa vyama vya siasa ambao wanapinga matokeo ya uchaguzi mkuu 2020. **PICHA: RENATHA MSUNGU.**

# Watanzania wahimizwa mshikamano

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

VIJANA na wajasiriamali wa Mkoa wa Dodoma, wamewaasa Watanzania kutokubali kugawanywa na watu wasioitakia mema Tanzania.

Kutokana na hilo, wamehimizwa kuendeleza umoja na mshikamano utakaosaidia kuwa na Taifa lenye kasi ya kimaendeleo.

Wakizungumza na waandishi wa habari jijini hapa, walisema uchaguzi mkuu tayari umepita kinachotakiwa ni kufanya kazi na wasikubali kujihusisha na vitu vitakavyowarudisha kimaendeleo.

Katibu wa Umoja wa vikundi vya vijana, watu wenye ulemavu pamoja na wanawake Mkoa wa Dodoma, Christopher Dioniz, alisema kuwa kila mtu anatakiwa kuwa mstari wa mbele kuilinda amani ya nchi wakati huu ambao uchaguzi umeshapita.

"Uchaguzi mkuu umepita lakini hivi sasa taifa lipo katika maandalizi ya kuapishwa kwa mshindi wa nafasi ya urais hivyo kila mmoja anatakiwa kuilinda amani yetu tuliyodumu nayo kwa miaka mingi," alisema.

Alisema Watanzania wasipokuwa wamoja na kulinda amani iliyopo watayumbishwa na watu wasiopenda maendeleo ya Tanzania.

"Katika awamu ya kwanza ya uongozi wa Rais Magufuli katika miaka mitano iliyopita sisi kama vijana tumenufaika na mikopo ya asilimia 10, isiyokuwa na riba, lakini pia kundi la vijana lilikuwa limesahaulika la walemavu, lakini katika awamu hii limewekwa kwenye utaratibu wa kupata mikopo," alisema Dioniz.

Vilevile, alisema kutokana na Tanzania kuingia katika uchumi wa kati katika awamu ya kwanza ya utawala wa Rais Magufuli, Watanzania wanatakiwa kuendelea kuchapa kazi, ili kufikia uchumi wa juu.

"Kwa namna ambavyo serikali ya awamu ya tano imepambana hadi kulifikisha taifa katika uchumi wa kati tunatumaini kuwa katika awamu ya miaka hii mitano mingine ya Rais Magufuli, tunatarajia kuingia katika uchumi wa juu," alieleza Dioniz.

Aidha, aliwataka wanasiasa walioshindwa katika uchaguzi huu kukubaliana na matokeo na kuacha kuhamasisha watu kufanya vurugu kwa kupinga matokeo.

"Uchaguzi huu umekuwa huru na haki hadi waangalizi wa kimataifa wametoa matokeo ambayo yanaonyesha haukua na shida kama ambavyo wanadai baadhi ya wanasisa nchini na kutaka kupinga matokeo," alisema.

Naye Mwenyekiti wa Wamachinga, Dodoma mjini Baraka Mrisho, aliwaomba viongozi wa dini kuendelea kuliombea taifa wakati huu ili amani iendelee kudumishwa nchini.

"Viongozi wa dini ndiyo wenye watu nchini, hivyo wanatakiwa kuhakikisha kuwa wanahubiri amani kwa wananchi wao ili wasirubuniwe na wanasiasa kuchafua amani iliyopo nchini," alisema Mrisho.



**HABARI MBEYA**

# Waandaliwa kupokea mbegu bora ya michikichi

**Na Grace Mwakalinga,** KYELA

WIZARA ya Kilimo imeiagiza Halmashauri ya Wilaya ya Kyela mkoani Mbeya kuwaandaa wakulima kupokea mbegu za kisasa za zao la michikichi kwa ajili ya kupanda kwenye mashamba yao.

Agizo hilo limetolewa jana na Mkurugenzi wa Maendeleo ya Mazao kutoka Wizara ya Kilimo, Nyasebwa Chimagu, wakati akiwa katika ziara ya kikazi wilayani Kyela, ili kufuatilia uzalishaji wa mazao ya kimkakati ikiwamo michikichi.

Chimagu alisema, serikali ina mkakati kabambe wa kuongeza uzalishaji wa zao hilo, ili taifa lijitosheleze kwa mafuta ya kula.

Alisema Wilaya ya Kyela ni miongoni mwa maeneo yenye uwezo wa kuzalisha zao hilo kwa wingi, lakini wakulima hawazalishi kwa tija kutokana na kutumia njia za kizamani na mbegu zisizokuwa na ubora.

"Serikali kupitia Wizara ya Kilimo imeanza kuhamasisha kilimo cha kisasa cha zao la michikichi wilayani Kyela, ili kulisaidia taifa lijitosheleze kwa mafuta ya kula, hivyo tunakusudia kuwaletea wakulima mbegu za kisasa na ni jukumu lenu kama wilaya kuwaandaa wakulima ili mbegu hizo zitakapokuwa tayari wazipande kwa wingi kwenye mashamba yao," alisema Chimagu.

Alisema kwa sasa mbegu bora za michikichi zinazalishwa mkoani Kigoma na tayari zimeanza kusambazwa katika maeneo yanayolima zao hilo na miongoni mwa maeneo ambayo mbegu hizo zitapelekwa ni wilayani Kyela.

Chimagu alisema kuwa serikali kupitia wakala wa mbegu za kilimo (ASA) pia imeanzisha shamba la mbegu bora za michikichi lililopo wilayani Mbozi ambalo litasaidia upatikanaji wa mbegu hizo kirahisi kwa wakulima wa Kyela.

Katika mwendelezo wa jitihada hizo, Halmashauri ya Wilaya ya Kyela kwa kushirikiana na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo nchini (TARI), Kituo cha Naliendele, mkoani Mtwara pia wameanzisha shamba la mbegu za michikichi kijiji cha Kikusyab, wilayani Kyela kwa ajili ya kuwasaidia wakulima kupata mbegu bora.

Ofisa Kilimo Kata ya Itope, Stella Mwakaje, alisema shamba hilo litakuwa ni shamba mama na la mfano kwa ajili ya upatikanaji wa mbegu za kisasa wilayani humo.

Kwa upande wake Ofisa Kilimo Wilaya, Kenneth Nzilan, alisema tayari waliandaa shamba lenye ukubwa wa ekari 13 lililopo Kata ya Makwale ambalo litatumika kama shamba darasa, ili kuwafundisha wakulima kilimo cha mazao ya michikichi na cocoa.



Mwajuma Mwakibinga akimwagilia shamba la mbegu za maharage la Taasisi ya Utafiti wa Kilimo nchini (TARI), Kituo cha Uyole jijini Mbeya. Shamba hilo limeandaliwa kwa ajili ya kuwasaidia wakulima kupata mbegu bora za maharage katika msimu ujao wa kilimo. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# TARI yaanza maandalizi teknolojia ya kisasa

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

TAASISI ya Utafiti wa Kilimo nchini (TARI), Kituo cha Uyole, imeanza maandalizi ya msimu mpya wa kilimo kwa kuandaa teknolojia za kisasa na mbegu bora za mazao mbalimbali kwa lengo la kuwasambazia wakulima.

Mkurugenzi wa TARI, Kituo cha Uyole, Dk. Tulole Bucheyeki, aliyasema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake, akidai kuwa maandalizi hayo ya teknolojia na mbegu za kisasa yatawafikia wakulima kwa wakati, ili wasipate usumbufu wa kuzitafuta.

Alisema mwaka huu wamezalisha mbegu bora ambazo zinahimili hali ya hewa ya aina zote na kwamba miongoni mwa mbegu walizoziandaa ni pamoja na maharagwe ambazo zitaanza kusambazwa kwa wakulima wenye uhitaji kwa ajili ya msimu ujao wa kilimo.

"Kujiandaa katika msimu ni jambo la maana sana tumeandaa teknolojia za kisasa na mbegu kwa lengo la kuwasaidia wakulima, ili wazitumie kipindi cha masika na tunaimani watazalisha mazao mengi na bora ambayo yatakidhi vigezo kwenye masoko ndani na nje ya nchi," alisema Dk. Bucheyeki.

Mratibu wa Utafiti na Ubunifu Kituo cha Uyole, Dk. Ndabhemeye Mlengela, alieleza kuwa jukumu la taasisi hiyo ni kuona wakulima wanapata teknolojia zilizo bora.

Alisema miongoni mwa huduma wanazozitoa kwa wakulima ni pamoja na kupima afya ya udongo kwenye mashamba ili kuhakikisha mazao ya wananchi yanastawi vizuri na kuzalisha kwa tija.

Alisema wakulima wa Nyanda za Juu Kusini wanapaswa kutumia kituo hicho kupata elimu ya uzalishaji teknolojia za kilimo na uzalishaji kwa kuzingatia kilimo biashara.

Mgunduzi wa mbegu bora za mazao wa kituo hicho, Kenneth Sabula, alisema sababu za kufanya maandalizi mapema ni kuepuka athari za mabadiliko ya tabia nchi kwa kuzalisha mbegu zinazohimili mabadiliko hayo.

# Kyela wauza tani 300,000 za cocoa

**Na Grace Mwakalinga,** KYELA

WAKULIMA katika Halmashauri ya Wilaya ya Kyela mkoani Mbeya, wamefanya mnada wa kuuza tani zaidi ya 300,000 za cocoa, huku bei ya zao hilo ikishuka kutoka Sh. 4,978 wiki iliyopita hadi Sh. 4,806 wiki hii.

Hata hivyo licha ya bei ya cocoa kushuka, bado bei ya cocoa wiki hii ipo juu ikilinganishwa na bei elekezi ya serikali ambayo ni shilingi 4,200 kwa kilo moja.

Wakizungumza kwenye mnada huo uliofanyika jana katika kijiji cha Itope, wakulima wa zao hilo walisema wanalazimika kuuza mazao yao ili waweze kupata fedha za kujikimu ingawa bei imeshuka.

Wakulima hao waliiomba serikali kuunda chombo huru kitakachokuwa kikiwajulisha wakulima mwenendo wa bei kwenye soko la dunia badala ya kuwategemea wafanyabiashara.

Mmoja wa wakulima hao, Ruson Mwakalebela, alisema hawawezi kuwaamini wafanyabiashara ambao ndio wanunuzi wa mazao yao, kwa vile wanaweza kushusha bei kwa makusudi ili waende kupata faida kubwa.

"Wafanyabiashara hawa wanaonunua mazao yetu ndio hawa hawa wanaotueleza kuwa bei kwenye soko la dunia imeshuka, mimi kama mkulima nitawaamini vipi wakati na wao wanataka wanunue kwa bei ndogo ili wakapate faida? Naiomba serikali iunde chombo huru ambacho ndio kitakuwa kinatujulisha sisi wakulima mwenendo wa bei ya mazao yetu kwenye soko la dunia," alisema Mwakalebela.

Mnada huo ulihudhuriwa na Mkurugenzi wa Maendeleo ya Mazao kutoka Wizara ya Kilimo, Nyasebwa Chimagu, ambaye alisema kuwa katika mfumo wa stakabadhi ghalani, wakulima hawapangiwi bei na wala hawalazimishwi kuuza mazao bila ridhaa yao.

Alisema serikali ina jukumu la kuhakikisha mkulima anapata bei inayoendena na gharama za uzalishaji na sio mtu mmoja au kikundi cha watu kuhodhi soko la mazao ya wakulima na kuwapangia bei wanayoitaka wao.

"Nasisitiza kuwa katika mfumo huu wa stakabadhi ghalani serikali hailazimishi wakulima kuuza mazao yao kwa bei wasiyoridhika nayo, ili mazao yauzike ni lazima wakulima wenyewe wakubali na kutoa uamuzi wa mwisho wa kuuza au kutouza, endapo hawaridhiki na bei iliyopo na wakakataa kuuza ni haki yao na kamwe kwa kufanya hivyo watakuwa hawajafanya kosa lolote," alisema Chimagu.

Alisema serikali itaingilia kati pale inapoona wakulima wanataka kupunjwa na watu ambao watapanga bei ndogo ya mazao isiyoendana na gharama za uzalishaji.



# Wananchi wapongezwa kwa utulivu kipindi cha uchaguzi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KAMATI ya Ulinzi na Usalama Mkoa wa Kusini Unguja imewapongeza wananchi wa mkoa huo, kwa kuimarisha hali ya amani na utulivu kabla na baada ya uchaguzi.

Akitoa taarifa ya tathmini ya hali ya usalama wakati wa uchaguzi katika mkoa huo, Mwenyekiti wa kamati hiyo ambaye ni Mkuu wa Mkoa huo, Ayoub Mohammed Mahmod, alisema hali ya usalama ilimarishwa na wananchi walijitokeza kwa wingi katika zoezi la upigaji kura bila ya hofu yoyote.

Alisema katika mkoa huo hakuna taarifa yoyote iliyoripotiwa ya mwananchi au kikundi cha watu kufanyiwa hujuma kwa sababu za uchaguzi huo.

Aliwataka wananchi kuendeleza utamaduni wa kutunza na kuimarisha amani na utulivu na shughuli zao za kujitafutia kipato, ili kuhakikisha wanapiga hatua za maendeleo.

Aliwapongeza Dk. John Magufuli na Dk. Hussein Ali Mwinyi, kwa kuchaguliwa kuwa marais na kwamba Mkoa wa Kusini utashirikiana nao katika hali ya kuendeleza maendeleo ya taifa.

Katika uchaguzi huo majimbo yote matano ya uchaguzi ya mkoa huo, yamechukuliwa na Chama Cha Mapinduzi kwa nafasi zote za ubunge, uwakilishi na udiwani.



Mamia ya wananchi wakifurahia baada ya Rais wa Awamu ya Nane wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Hassan Mwinyi, kuapishwa rasmi jana, kwenye Uwanja wa Aman. **PICHA: MARTIN KABEMBA**.

# H'shauri yapania mapinduzi kielimu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

HALMASHAURI ya Wilaya ya Kusini Unguja, imedhamiria kuondoa tatizo linalowakumba walimu wa shule za maandalizi na msingi katika wilaya hiyo, ili kuleta mapinduzi ya kielimu wilayani humo.

Akizungumza baada ya kukamilika kwa mafunzo ya uongozi yaliyoandaliwa na halmashauri hiyo kwa walimu wakuu na walimu wakuu wasaidizi wa wilaya hiyo katika shule ya Kitogani.

Mkurugenzi wa halmashauri hiyo, Kassim Abu Mtoro, alisema endapo walimu watasimamia vyema majukumu yao na kufuata miongozo inayotolewa na Wizara ya Elimu itasaidia kukuza kiwango cha elimu kwa wanafunzi wa shule hizo.

Alisema halmashauri itafanya jitihada za kuwapatia walimu stahiki zao za likizo, fedha za ruzuku za uji pamoja na posho za nauli ili kuongezea ari ya hamasa ya ufundishaji kwa wanafunzi.

Alisema jumla ya Sh. milioni 13 zimetengwa kwa ajili ya kuwalipa walimu fedha za likizo.

Pia, alisema ni matarajio yake walimu wataongeza juhudi na mbinu za ufundishaji ili kuhakikisha viwango vya ufaulu kwa wanafunzi vinaongezeka.

Kwa upande wake Ofisa Elimu wa halmashauri hiyo, Hamid Abdulhamid Khamis, alisema katika kuimarisha elimu kwa ngazi za awali wamewataka walimu kuandikisha wanafunzi wa darasa la kwanza ambao wameshajua kusoma, kuandika na kuhesabu kwa wale wanaotokea shule za maandalizi ili kupunguza wimbi la wanafunzi wa msingi na sekondari wasiojua kusoma na kuandika.

Washiriki walisema mafunzo hayo yamewapa ufanisi wa kuongeza kasi ya utoaji elimu kwa wanafunzi, huku wakiomba kutatuliwa matatizo yanayozikabili shule zao.

Katika mafunzo hayo mada mbalimbali zilijadiliwa ikiwamo ya majukumu ya walimu wakuu na wasaidizi wao katika ngazi ya shule pamoja na mada ya utumishi wa umma.

# CCM Z'bar yasema uchaguzi ulikuwa huru na haki

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

CHAMA Cha Mapinduzi Zanzibar, kimesema uchaguzi mkuu uliofanyika Oktoba 28, mwaka huu ulikuwa huru na wa haki licha ya baadhi ya watu kujaribu kufanya vitendo vya uvunjifu wa amani.

Naibu Katibu Mkuu wa CCM, Abdallah Juma Mabodi, alisema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu tathmini ya zoezi la uchaguzi kabla ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, kuapishwa jana viwanja vya Amani.

"Tathmini yetu kama chama, uchaguzi mkuu ulikuwa huru na wa haki tumeshuhudia wananchi wakijitokeza kupiga kura katika mazingira ya amani na kazi ya majumuisho na kuhesabu kura imefanyika katika mazingira ya uwazi," alisema Mabodi.

Alisema uchaguzi una hatua mbalimbali ikiwamo uandikishaji wa wapigakura, kampeni, upigaji wa kura na utoaji wa matokeo ya uchaguzi na yote hayo yamefanyika kwa uwazi ikiwamo kushirikishwa kwa wadau wa uchaguzi.

Hata hivyo, alisema kwamba kama mtu ana malalamiko au kinyongo, mlango upo wazi kwa kuwasilisha malalamiko katika vyombo vya sheria na sio kuwataka wananchi kuandamana bila ya kujali madhara yake katika suala la kulinda amani na umoja wa kitaifa.

"Hakuna haki inayopatikana kwa maandamano kama una malalamiko kuna vyombo vya kisheria vya kusikiliza malalamiko, madhara ya kuandamana ni makubwa katika kulinda amani na ustawi wa wananchi wake.

Kuhusu Serikali ya Umoja wa Kitaifa, alisema suala hilo lipo kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar na Chama Cha Mapinduzi hakina tatizo na kuundwa kwa serikali hiyo baada ya kumalizika kwa uchaguzi mkuu mwaka huu.

Alisema CCM imepata ushindi mkubwa kutokana na utekelezaji mzuri wa ilani ya uchaguzi uliofanywa na serikali ya awamu ya saba pamoja na kampeni nzuri zilizofanywa na mgombea ikiwamo kuyafikia makundi mbalimbali na kunadi sera zake mbali ya ilani ya uchaguzi ya mwaka 2020\2025.

"Kampeni zetu zilikuwa za kisayansi tumeweza kukutana na makundi mbalimbali wakiwamo wavuvi, wajasiriamali, mama lishe, wafugaji, wafanyabiashara, walimu na asasi zingine za kiraia," alisema Mabodi.

Alisema kwamba wapinzani hawakuwa na hoja za msingi katika kunadi sera zao, pia wameshindwa kuyafikia makundi mengine ndio maana wameshindwa vibaya katika uchaguzi na baadhi ya vyama kutumia muda mwingi kushughulikia migogoro ya uongozi badala ya kujenga vyama vyao.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

Nipashe

NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI

KWA BEI NAFUU SANA

Nipashe

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**Probate and Administration cause No .60 Of 2020**
**In the matter of the Estate of the late THEOPHIL PETER NJELEKA of Area "E" within Dodoma City.**

And
In the matter of Application for letters of Administration by **CHRISTINA PETER KAUKI** and **PATRICK PETER NJELEKA.**

**GENERAL CITATION**

(Rule 75 of Probate Rules GN 369 of 1963)

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before **23 day of 11, 2020.**
Dated at Dodoma this 2 day of **NOVEMBER, 2020.**

RESIDENT MAGISTRATE

## KUITWA SHAURINI

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA YA KINONDONI**
**MWANANYAMALA**

SHAURI LA MADAI NAMBARI 31 LA 2020
**DEOGRATIUS RUTABANA** MWOMBAJI DHIDI YA
**FLORENSO KILAMBATA** MJIBU MAOMBI
WITO KUITWA SHAURINI
MDAIWA POPOTE ULIPO/MLIPO

**DEOGRATIUS RUTABANA** amefungua shaurimbele ya baraza la ardhi na nyumba lililopo kinondoni (mwananyamala) . shauri husika limepangwa kutajwa tarehe **2/12/2020 saa 3;00 asubuhi** ,mbele ya **Mh S.H.WAMBILI.** Hivyo basi unatakiwa kuleta utetezi wako ndani ya siku ishirini na moja (21) kuanzia tarehe ya tangazo hili kutolewa. Vielelezo vyote vya kesi vinapatikana katika masijala ya tangazo la baraza la ardhi na nyumba kinondoni. Endapo hautatekeleza haya,shauri litasikilizwa upande mmoja na hukumu kutolewa.
Imetolewa nakutiwa sain na mhuri wa baraza hii leo tarehe **02/11/2020**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**DONATHA P. PAULO**
ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA **SPACIO** YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 927 CYP**. YOYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI.
TAARIFA YA POLISI:
**DAR/MBU/RB/761086/2020.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MSN LOGISTICS LIMITED**
Wanatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TIPPER** yenye namba za usajili **T 820 DNY** chasis namba **YS2P6X40002007669** yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
Polisi taarifa
**DAR/KIJ/RB/771364/2020**

Uza,
Chenye
Thamani
Kubwa Kwa
Kutangaza
Nasi
Kwa Bei Poa
Tupigie
0782253676

## USIMAMIZI WA MIRATHI

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika mahakama ya mwanzo**
**MJINI-MOROGORO**

Usimamizi wa mirathi **No;330/2020**
Ombi la **MICHAEL METHOD GOMBO**, Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu **METHODY VALENTINE GOMBO**.Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe **09/11/2020** kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe **02/11/2020.**

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**MSAFIRI BATHOROMAYO NZILANO**
anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye namba za usajili
**MC 842 BLH.**
Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu.
Taarifa ya polisi
**MB/MB/RB/738395/2020.**

## USIMAMIZI WA MIRATHI

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2 Katika mahakama ya mwanzo**
**MJINI-MOROGORO**

Usimamizi wa mirathi **No;329/2020**
Ombi la
**PROF GERALD CLAUDIUS MONELA**,
Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu **EDITH GERALD MONELA**.Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe **02/12/2020** kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe **02/11/2020**

## USIMAMIZI WA MIRATHI

**Katika Mahakama ya Mwanzo Uchira**
**USIMAMIZI WA MIRATHI NO, 15/2020**
Ombi La
**John Malamia Msaki**
Usimamizi wa mirathi ya marehemu
**Malamia Ngareiya Msaki Mrumeni**

Kwa: **YEYOTE ANAYEHUSIKA**
Watu wote mnaodai kuwa na haki na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe **12/11/2020**
Kabla huyu mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Wosia wa marehemu upo Mahakamani waweza kukaguliwa

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KIMATAIFA

# Kenya yazindua bima ya afya kwa raia wake wote

**Nairobi, KENYA**

SERIKALI ya Kenya imezindua mpango wa kutoa bima ya afya kwa kila raia wake, ili kuwawezesha kupata matibabu kwa bei nafuu.

Rais wa nchi hiyo, Uhuru Kenyatta alisema mpango huo ni sehemu ya ajenda zake nne za maendeleo kwa ajili ya raia wa Kenya.

Uzinduzi huo unajili baada ya miaka miwili ya kufanyiwa majaribio yaliyokuwa yakiendelea katika miji minne ya Kisumu, Machakos, Nyeri na Isiolo.

Serikali ya Kenya ilisema kwamba imejitolea kufanya uwekezaji wa kimkakati katika sekta ya afya ili kuhakikisha kwamba raia wote wa nchi hiyo wanapata huduma muhimu za afya wanazohitaji ifikapo mwaka 2022.

Raia wa Kenya milioni moja kutoka jamii maskini, watasajiliwa kwa njia ya digitali katika awamu ya kwanza.

Katika mkutano wa wadau mjini Mombasa, uliowaleta pamoja magavana na viongozi wengine wa serikali kuu, ili kutathmini hatua muhimu zilizofikiwa katika mpango wa majaribio.

Imeelezwa kwamba kuna nafasi kubwa kwa mpango huo kutekelezwa kwa haraka katika majimbo yote ya Kenya, 47.

Rais Kenyatta alitoa wito kwa kila raia wa Kenya kuunga mkono mpango huo, akitoa mwito kwa bunge kupitisha kwa haraka sheria kuulinda.

"Msicheleweshe mpango huu kwa mijadala isiyofaa. Sote tunajua tunakotaka kwenda. Huu sio wakati wa kutuonyesha uwezo wako katika mijadala," alisema Rais Kenyatta.

Kenyatta alionya wasimamizi wa mpango huo kutofuja fedha za umma zinazotakiwa kufanikisha utekelezwaji wake.

"Tuna nafasi ya kurekebisha tatizo mara moja na mwisho kabisa. Ikiwa wale waliopewa jukumu la kushughulikia fedha hizi hawatafanya hivyo kwa uangalifu na tahadhari, watajuta kwa maisha yao yote."

Watu milioni 22 wamesajiliwa kwa mfumo wa bima ya afya ya kitaifa NHIF, ambao wasimamizi wake wanasema watatumia taarifa za waliosajiliwa kuharakisha ufanisi wa mfumo mpya ambao umezinduliwa. **VOA**



Rais wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Félix Tshisekedi, jana, alitangaza mashauriano ya umoja wa kudumu. Mashauriano hayo yameanza kutekelezwa, yakilenga kumaliza mkwamo wa shughuli za serikali kutokana na tofauti za Joseph Kabila na muungano wa FCC. **PICHA/AFP**

# Ouattara aongoza katika hesabu ya kura Ivory Coast

**Abidjan, Ivory Coast**

RAIS wa Ivory Coast, Alassane Ouattara, anaongoza katika hesabu ya kura katika uchaguzi uliofanyika.

Ouattara mwenye umri wa miaka 78, anagombea mhula wa tatu madarakani licha ya maandamano makubwa yaliyotokea kupinga hatua yake ya kugombea mhula mwingine.

Hadi jana ripoti zilieleza kwamba, Ouattara alikuwa amepata ushindi mkubwa katika wilaya 26 kati ya 108.

Rais Ouattara anatarajiwa kushinda muhula mwingine baada ya wapinzani wake kuwaambia wafuasi wao kutoshiriki uchaguzi huo, wakidai kwamba sio uchaguzi unaokubalika kisheria.

Ouattara alisisitiza kwamba katiba mpya iliyopitishwa mwaka 2016, inamruhusu kugombea muhula mwingine madarakani.

Watu 30 wameuawa katika maandamano ya kupinga Ouattara kugombea muhula mwingine madarakani.

Watu watano waliripotiwa kuuawa Jumamosi wakati uchaguzi ukiendelea.

Katika taarifa ya pamoja, wagombea wa upinzani akiwamo aliyekuwa Rais Henri Konan Bedie na aliyekuwa Waziri Mkuu, Pascal Affi N'Guessan walisema kwamba watu 30 wameuawa. Hawakutoa taarifa zaidi.

"Upinzani unaitisha maandamano kuzuia udikteta huu," alisema Affi.

Alisema kwamba asilimia 10 ya wapiga kura wameshiriki katika zoezi la upigaji kura, lakini hajatoa ushahidi wowote.

Hakuna taarifa rasmi kuhusu idadi ya watu ambao wamepiga kura, lakini kundi la waangalizi wa ndani limesema kwamba asilimia 23 ya vituo vya kupigia kura havikufunguliwa baada ya kuzuiwa na wafuasi wa upinzani waliofunga njia kuelekea kwenye vituo hivyo na kuwatishia maofisa wa tume ya uchaguzi.

Watu 3,000 waliuawa katika ghasia za baada ya uchaguzi mwaka 2010 - 2011 nchini Ivory Coast.

**VOA**

## Azerbaijan yashambulia msafara Jeshi la Armenia

**Baku, AZERBEIJAN**

JESHI la Azerbaijan limeshambulia msafara wa Jeshi la Armenia katika operesheni iliyoanza ya kuokoa eneo lake kutoka kwenye uvamizi.

Katika taarifa iliyotolewa na Wizara ya Ulinzi ya Azerbaijan, ilisema kuwa mnamo Oktoba 31, mwaka huu, saa 11 jioni harakati za msafara wa Jeshi la Armenia kuelekea Hocavend, zilligunduliwa. Katika taarifa hiyo, iliripotiwa kuwa msafara huo ulivurugwa kwa kupigwa risasi na mizinga kwa wakati mmoja.

Imebainika kuwa baadhi ya magari ya Jeshi la Armenia yaliharibiwa na wanajeshi waliangamizwa katika shambulizi hilo.

Wizara hiyo pia imerusha picha za shambulizi hilo na umma.

Inasemekana kwamba Arayik Harutyunyan, mkuu wa kile kinachoitwa utawala wa Armenia huko Nagorno-Karabakh, pia alikuwapo kwenye msafara uliopigwa risasi.

**TRT**

## Mkuu wa WHO ajiweka karantini

**Washington, MAREKANI**

MKUU wa Shirika la Afya Duniani (WHO), Tedros Ghebreyesus, ameanza kujitenga baada ya kukutana na mtu aliyebainika kupata maambukizi ya virusi vya corona.

Ghebreyesus alisema yeye binafsi hakuwa na dalili za corona.

"Mtu niliyekutana naye hivi karibuni amebainika kuwa na maambukizi ya virusi vya corona. Niko sawa kuwa sina dalili zozote, lakini nitajitenga kwa siku kadhaa zijazo, kama ilivyo katika mwongozo wa WHO na kufanya kazi nyumbani," ameandika kwenye ujumbe wa Twitter.

"Wafanyakazi wenzangu wa WHO na mimi tutaendelea kushirikiana na wengine kuokoa maisha na kulinda maisha ya walio hatarini," aliongeza. Ghebreyesus mwenye miaka 55, alikuwa Waziri wa Afya, nchini Ethiopia, alisema "ni muhimu sana kufuata mwongozo wa Wizara ya Afya".

Kwa njia hii, ndio tutafanikiwa kukabiliana na usambazaji wa ugonjwa wa Covid-19 kukabiliana na kirusi hiki, na kulinda mifumo ya afya."

**BBC**

## Trump, Joe Biden kampeni lala salama

**Michigan, MAREKANI**

RAIS Donald Trump wa Marekani na mpinzani wake kutoka Chama cha Democratic, Joe Biden, jana, walifanya mikutano kwenye majimbo yenye ushindani mkali kabla ya kufanyika uchaguzi wa rais leo.

Akizungumza kwenye jimbo lenye mchuano mkali la Michagan, Trump aliwaonya wafuasi wake kuwa, Biden atazifunga shughuli za kawaida kama njia ya kukabiliana na janga la virusi vya corona, mbinu ambayo Trump alidai inavuruga uchumi.

Kwa upande wake Biden, aliyehutubia mjini Philadelphia, alirejea matamshi yake ya kumshambulia Rais Trump kwa jinsi anavyoshughulikia janga la virusi vya corona, ambalo limesababisha vifo vya zaidi ya watu 230,000 nchini Marekani.

Wagombea wote walitumia siku za mwisho za kampeni kufafanua misingi ya sera na ilani, huku kura za maoni ya umma zikionyesha Joe Biden anaongoza dhidi ya Trump, anayewania muhula wa pili kwenye uchaguzi huo wenye ushindani mkali. **DW**



# PARTEY
## KAMA VIEIRA - KEANE

**Manchester, ENGLAND**

KAMA kuna yeyote ambaye ni mgumu kumvutia pengine anaweza kuwa Roy Keane, hata hivyo mkongwe huyo wa Manchester United, hakuweza kuficha kuvutiwa kwake na Thomas Partey baada ya kumtazama kiungo huyo akiichezea Arsenal Jumapili dhidi ya klabu yake hiyo ya zamani.

Kiwango bora kilichoonyeshwa na Partey, pia kilimfanya Keane kumfananisha nyota huyo raia wa Ghana na kiungo wa zamani wa Arsenal, Mfaransa Patrick Vieira.

Partey alionyesha kiwango chake cha uchezaji bora wa mechi dhidi ya Manchester United, na kuwafunika viungo kama Bruno Fernandes, Paul Pogba na Scott McTominay.

Keane aliiambia Sky Sports: "Wakati unamtazama mchezaji mubashara, hivyo ndivyo unavyoweza kumwelezea. Unavyomtazama zaidi yeye [Thomas Partey], zaidi natamani angekuwa kwenye safu ya kiungo ya Man United.

"Nadhani mtoto huyu amepata nafasi ya kulinganishwa na kile Patrick [Vieira] alikuwa akifanya [hapo Arsenal]," alisema.

Katika mechi hiyo ambayo ilipigwa Uwanja wa Old Trafford juzi, Arsenal ilishinda kwa bao 1-0 kwa mkwaju wa penalti iliyozamishwa nyavuni na Pierre-Emerick Aubameyang dakika ya 69.

Partey ambaye amejiunga na Arsenal majira haya ya joto akitokea Atletico Madrid kwa dau la pauni milioni 45, alitangazwa mchezaji bora wa mechi hiyo ambayo Manchester United ilikubali kipigo cha kwanza nyumbani dhidi ya Gunners tangu mwaka 2006.

## BARCELONA SASA KUMUUZA TER STEGEN




**BARCELONA, Hispania**

BARCELONA imeripotiwa kutaka kumuuza golikipa wake, Marc-Andre ter Stegen kwenda kujiunga na Bayern Munich, kwa mujibu wa TodoFichajes.

Ter Stegen mwenye umri wa miaka 28, alisaini mkataba mpya na miamba hao wa LaLiga mwezi uliopita, lakini majaliwa yake yanaonekana kutojulikana.

Na sasa Barcelona wanafikiria kumuuza Ter Stegen kwenda kule Bayern Munich.

Ripot zinasema kwamba, Bayern inamtaka Ter Stegen ili kuchukua nafasi ya Neuer mwenye umri wa miaka 34, na ada yake inaweza kuwa euro milioni 80.

Ter Stegen, ambaye mkataba wake unamalizika mwaka 2025 na Neuer wanachukuliwa kama magoli kipa bora zaidi duniani kwa sasa.

Katika msimu uliopita wa Ligi ya Mabingwa Ulaya, Neuer alikuwa na wastani wa ubora wa asilimia 77.1 - nyuma ya Andre Onana (80) na Alex Meret (79).

## MOURINHO AKUNWA KIWANGO CHA BALE

**LONDON, England**

JOSE Mourinho amemsifia Gareth Bale kwa kuonyesha kiwango bora wakati akifunga bao la ushindi dhidi ya Brighton and Hove Albion na anasubiri kusikia Real Madrid wanasemaje kwa ubora wake.

Bale hilo lilikuwa bao lake la kwanza kwa Tottenham tangu alipojiunga tena na Spurs kwa mkopo akitokea kwa mabingwa wa LaLiga, Madrid, Septemba na alikuwa nguzo ya ushindi wa 2-1 dhidi ya Brighton, Jumapili.

Harry Kane, alianza kufunga bao la kwanza kwa mkwaju wa penalti katika mchezo huo.

Na Mourinho aliwaambia waandishi wa habari kwamba, ameridhishwa na kiwango cha Bale na sasa anasubiri kusikia kutoka kwa Zinedine Zidane atasema nini kuhusu kiwango cha mchezaji huyo.

"Kwa wiki sasa, amekuwa akiimarika," alisema Mourinho akiwaambia waandishi wa habari.

"Nafurahi kumuona akicheza na takwimu zake zinaonyesha wazi kwamba yupo kwenye kiwango cha kuvutia zaidi kwa sasa."



HABARI MICHEZO

# RONALDO KAFANYA KAZI YAKE JUVE- PIRLO




**TURIN, Italia**

CRISTIANO Ronaldo alifanya "kazi yake" wakati alipoifungia Juventus mabao mawili dhidi ya Spezia, amesema kocha wake, Andrea Pirlo.

Baada ya kukutwa na virusi vya corona, Ronaldo alikosa mechi nne za Juve, lakini alirudi dimbani na mabao mawili akitokea benchi kwenye mchezo wa Jumapili wa ushindi wa 4-1.

Na Pirlo aliwaambia waandishi wa habari baada ya mchezo huo kuwa Ronaldo alifanya kazi yake vizuri baada ya kuingia katika dakika ya 56.

"Tulitengeneza nafasi nyingi kipindi cha kwanza, ilikuwa ni aibu tulikuwa sawa kipindi cha kwanza baada ya kutengeneza nafasi nyingi," alisema.

"Tunatakiwa kuwa makini zaidi tukiwa golini, kwa sababu tulipata nafasi nyingi, lakini hatukuweza kuzitumia.

"Lakini Cristiano alipoingia uwanjani alifanya kazi yake na hilo ndilo linalotakiwa kwa mchezaji.

"Hatuangalia msimamo wa ligi ilivyo kwa sasa, kwa sababu tunajua kwamba tulipoteza pointi katika mechi kadhaa."

## GABRIEL AKUNWA NA VAN DIJK LIVERPOOL

**LONDON, England**

BEKI wa Arsenal, Gabriel Magalhaes, amesema amekuwa akimkubali sana beki Virgil van Dijk na anatamani kucheza dhidi yake pamoja na Sergio Aguero.

Gabriel amesajiliwa na Arsenal msimu huu akitokea katika Klabu ya Lille ya Ufaransa kwa kiasi cha pauni milioni 27.

Beki huyo raia wa Brazil, Gabriel amesema: "Katika mabeki ambao nawakubali sana ni Van Dijk na nimefurahi nimecheza dhidi yake jambo ni changamoto kwangu pia.

"Pia nimecheza dhidi ya Man City japo tulipoteza ila tulijifunza mengi kutoka kwao. Nikacheza dhidi ya mchezaji bora Aguero ambaye mabeki wengi wanatamani kucheza naye na kujua ni staili ipi wanaweza kucheza naye.

"Tumeshacheza na timu kubwa na tumejifunza mengi na kuangalia wapi tunatakiwa kufanya marekebisho hasa tunapokuwa uwanjani.

"Lakini kwa ujumla ligi hii ina ushindani sana kuliko kawaida na ndiyo maana nilichagua kuja Ligi Kuu ya England.

Hata hivyo, Gabriel alieleza kuwa wakati anakipiga katika Ligue 1 straika ambaye alikuwa akimsumbua zaidi alikuwa ni Kylian Mbappe wa PSG.




## FERNANDES ATABIRI MAKUBWA NA POGBA

**MANCHESTER, England**

BRUNO Fernandes amesema ana "mahusiano mazuri" na mchezaji mwenzake, Paul Pogba na anaamini wanaweza kufanya vitu vikubwa zaidi kwa Manchester United.

Fernandes amekuwa na kiwango cha kuvutia pale Old Trafford tangu atue akitokea Sporting CP, Januari.

Kiungo huyo amekuwa na kiwango cha kuvutia zaidi hapo United na alikuwa na mchango mkubwa kwa kikosi hicho kilipomaliza nafasi ya tatu kwenye msimamo wa Ligi Kuu msimu uliopita.

Hata hivyo, kikosi hicho cha kocha, Ole Gunnar Solskjaer msimu huu kimekuwa kinasuasua.

Lakini Fernandes anajiamini kwamba timu hiyo inaweza kuimarika zaidi kwa siku zinazokuja.

"Tuna mahusiano mazuri sana na Pogba," alisema Fernandes akiiambia Sky Sports. "Na naamini tuna nafasi ya kufanya makubwa zaidi kwa siku zinazokuja.

## HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# ARTETA ACHAMBUA REKODI ARSENAL, AUBAMEYANG UTD

Tulijiandaa zaidi ya Man United, tungeweza kufunga mabao mara mbili katika kipindi cha kwanza, lakini...

**LONDON, England**

MIKEL Arteta ameelezea rekodi Arsenal na Pierre-Emerick Aubameyang waliyoiweka wakati wakiibuka na ushindi wao wa kwanza wa Ligi Kuu katika dimba la Old Trafford tangu mwaka 2006, kuwa ni kutokana na wachezaji wake kujiandaa zaidi kuliko Manchester United.

Arsenal walionekana kuwa bora zaidi ya 'Mashetani Wekundu' hao na kuibuka na ushindi wa bao 1-0 lililofungwa na Aubameyang kwa mkwaju wa penalti kipindi cha pili, baada ya Paul Pogba kumfanyia faulo, Hector Bellerin ndani ya boksi.

Kwa bao hilo Aubameyang ameweka rekodi ya kuwa mchezaji wa kwanza Arsenal kuzamisha mkwaju wa penalti nyavuni katika Uwanja wa Old Trafford kwenye Ligi Kuu England - hakuna penalti yoyote ya hivi karibuni iliyozama kimyani kati ya mbili zilizopigwa na Gunners katika uwanja huo (Robin Van Persie mwaka 2011 na Gilberto Silva mwaka 2006).

Lakini Arteta ameweka rekodi ya kuwa kocha wa kwanza katika historia ya Arsenal kushinda mechi zote mbili za ufunguzi dhidi ya United, baada ya Herbert Chapman msimu wa mwaka 1925-26.

Na raia huyo wa Hispania amejisifia kwamba, walikuwa na uhakika wa ushindi huo.

"Nimefurahishwa na ushindi kwa sababu wachezaji wangu walijiandaa kwa hili," alisema Arteta akiiambia BBC.

"Unatakiwa kushinda katika mapambano yako na ndivyo ilivyotokea leo (juzi).

"Nilitaka kuhakikisha kwamba tunapata ushindi na wachezaji walionyesha ari kubwa ya kutafuta ushindi na mwisho wa siku tukapata ushindi.

"Tungeweza kufunga mabao mara mbili katika kipindi cha kwanza, lakini hatukutumia nafasi zetu vizuri."

Penalti ya Aubameyang ilimfanya kumaliza ukame wa mechi tano bila kufunga goli kwenye Ligi Kuu na Arteta ana matumaini straika huyo wa kimataifa wa Gabon sasa ataendelea kufunga.

"Nina furaha kwamba, Aubameyang amefunga, kwani maswali yalikuwa mengi kuhusu kufunga mabao.

"Alifunga bao muhimu na naamini ataendelea kufunga katika mechi zinazokuja."

## KWA UFUPI

**ALABA KUONDOKA BAYERN**
WAKALA Pini Zahavi amesema mlinzi wa Bayern Munich, David Alaba, ataondoka Januari, huku klabu za Real Madrid, Juventus na Inter Milan zikionyesha nia ya kutaka kumsajili raia huyo wa Austria mwenye umri wa miaka 28. ***(Calciomercato)***

**MILAN YAMTAKA EMERSON**
AC Milan imemfanya mlinzi wa Barcelona, Emerson mwenye umri wa miaka 21, ambaye anacheza kwa mkopo katika klabu ya Real Betis, kuwa mchezaji wanayemhitaji zaidi msimu ujao. ***(Todofichajes)***

**GATTUSO AMTAJA JAMES BOND**
KOCHA wa Napoli, Gennaro Gattuso, amebainisha kuwa nyota James Bond Sir Sean Connery, aliyefariki dunia Jumamosi, alijaribu wakati mmoja kumshawishi kutoondoka Rangers. ***(Sky Sports)***

**SARRI ATAJWA FIORENTINA**
KOCHA wa zamani wa Chelsea, Maurizio Sarri, anaongoza katika orodha ya watakaochukuwa nafasi ya Bappe Lachini kama atafukuzwa kule Fiorentina. ***(Calciomercato)***

**JESUS AREJEA MAN CITY**
MSHAMBULIAJI wa Brazil, Gabriel Jesus, mwenye umri wa miaka 23, ameonyesha picha yake akiwa mazoezini na kikosi cha Manchester City baada ya kuwa nje ya dimba akiuguza majeraha. ***(Manchester Evening News)***

**WOLVES WAMTAKA SPENCE**
KLABU ya Wolves ina mpango wa kumnyakua beki wa kulia wa Middlesbrough, Djed Spence, mwenye umri wa miaka 20, wakati wa dirisha la usajili la Januari. ***(Teamtalk via Birmingham Mail)***

**INTER KUMUUZA ERIKSEN**
KLABU ya Inter Milan iko tayari kumuuza kiungo wa kati wa Denmark, Christian Eriksen, huku AC Milan, Roma na Lazio zikionyesha nia ya kumwania nyota huyo wa zamani wa Tottenham Hotpur mwenye umri wa miaka 28. ***(Calciomercato)***

**NEYMAR YUPO SANA PSG**
NEYMAR ameiambia klabu cha Paris St-Germain kuwa anataka kubaki klabuni hapo na mazungumzo ya makubaliano mapya ya mkataba yameanza. ***(Foot Mercato, via Sunday Mirror)***

**JONES HOFU TUPU BURNLEY**
PHIL Jones mwenye umri wa miaka 28, anahofia kwamba uhamisho wa mkopo kutoka Manchester United hadi Burnley Januari upo hatarini kwa sababu klabu hiyo huenda ikanunuliwa. ***(Daily Star Sunday)***

**ISCO HUYOOO EVERTON**
MSHAMBULIAJI wa Hispania na Real Madrid, Isco mwenye umri wa miaka 28, anafuatilia kwa karibu kukutana na aliyekuwa kocha wake, Carlo Ancelotti, na aliyekuwa mchezaji mwenza, James Rodriguez pale Everton. ***(Sunday Mirror)***

**PEREIRA NA MATUMAINI LEICESTER**
MLINZI wa kulia wa Ureno, Ricardo Pereira, mwenye umri wa miaka 27, ambaye amefanyiwa upasuaji wa goti, ana matumaini atarudi tena kuichezea Leicester City ndani ya wiki sita zijazo. ***(O Jogo, via Independent)***

**JUVENTUS YAMTAKA FATI**
JUVENTUS ilijaribu kumsajili mshambuliaji wa Barcelona na Hispania, Ansu Fati mwenye umri wa miaka 17, katika dirisha la usajili la majira ya joto lililopita. ***(Calcio Mercato)***

**GRIEZMAN KUONDOKA BARCA**
MSHAMBULIAJI wa Barcelona, Antoine Griezmann mwenye umri wa miaka 29, yupo tayari kupunguza mshahara wake ili aondoke klabuni hapo na kujiunga na klabu nyingine. ***(Marca)***

HABARI MICHEZO

# GWAMBINA YATAMBA KUISIMAMISHA YANGA

**Na Saada Akida**

WAKATI leo wakiikaribisha Yanga katika Uwanja wao wa Gwambina uliopo Misungwi, Mwanza, Kocha Mkuu wa Gwambina FC, Novatus Fulgence, ametoa tahadhari kwa wapinzani wao hao akiwataka kamwe wasijidanganye kwamba wana kikosi imara.

Akizungumza na gazeti hili kwa njia ya simu jana, Fulgence alisema kwa upande wao hawaihofiii Yanga kwa sababu kikosi chao kipo vizuri na ana imani watakuwa timu ya kwanza kuwazuia katika harakati zao za kuondoka na pointi tisa Kanda ya Ziwa.

Alisema Yanga wasijidanganye kwamba wako vizuri zaidi na kujihakikisha kila mechi wataondoka na pointi tatu katika mechi za ligi hiyo inayoshirikisha timu 18 msimu huu.

"Nimesikia wanasema wamejipanga kuondoka na pointi tisa Kanda ya Ziwa, wamefanikiwa kupata sita, ila kwangu haitakuwa rahisi kama wanavyofikiria, pia haijawahi kutokea kuondoka na alama hizo hata wawe fiti kiasi gani," alisema Fulgence.

Alisema amewaangalia wapinzani wao hao, na ana imani Yanga itakapokutana na timu hiyo iliyojipanga na kukaa muda mrefu itakuwa vigumu kupata pointi tatu.

"Kwa upande wangu nina imani mechi yetu dhidi yao itakuwa ya ushindani mkubwa, kwani sitahofia wachezaji wao, akiwamo Michael Sarpong na Tonombe Mukoko kwani ukiangalia kasi yao ya ufungaji haiko vizuri kama ilivyo kwa nyota wangu Meshack Abrahamu," alisema Fulgence.

Tonombe na Sarpong kila mmoja amecheka na nyavu mara mbili wakati Abrahamu yeye akiwa na mabao manne hadi sasa kwenye orodha ya wafungaji vinara inayoongozwa na Prince Dube wa Azam FC ambaye ameshatikisa nyavu mara sita.

TUMEWASHIKA...



Wachezaji wa Ruvu Shooting wakishangilia moja kati ya mabao yao matatu wakati wakiibuka na ushindi wa 3-1 dhidi ya Coastal Union ya Tanga katika mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara uliopigwa Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam juzi. **MPIGAPICHA WETU**

# Bodi ya Ligi yajivunia ubora Ligi

**Na Adam Fungamwango**

BODI ya Ligi nchini (TPLB), imeeleza kuridhishwa na mwenendo wa Ligi Kuu Tanzania Bara inavyokwenda na kuongeza kuwa kumekuwa na ushindani mkubwa, huku pia malalamiko ya viwanja vibovu yakiwa yamepungua.

Afisa Mtendaji Mkuu wa Bodi hiyo, Amasi Kasongo, alisema jana kuwa msimu huu mpaka sasa wameshuhudia ligi yenye upinzani mkali, huku timu inayojipanga vema ndiyo inashinda na haijalishi ipo nyumbani ama ugenini.

"Sisi kama bodi tunaendelea kuridhishwa na namna ligi inavyokwenda mpaka sasa. Ni tofauti na ilivyokuwa misimu kadhaa nyuma. Leo unaona timu iliyojipanga vizuri inashinda hata ugenini, na kuna ushindani mkali sana, timu zimekuwa hazipishani sana kiuwezo uwanjani, na hata safari hii tumeweza kukakazia sana kanuni ya viwanja," alisema.

Alisema msimu huu wamekuwa makini mno na viwanja kiasi kwamba hata vile ambavyo vilionekana miaka mingi kushindikana kukarabatiwa, safari hii wamevifanya kukarabatiwa na kuchezeka vema. "Viwanja vingi sasa vinachezeka, ni kwa sababu tulitilia mkazo na hili tutaendelea nalo," alisema Kasongo.

Mpaka sasa jumla ya mechi 79 zimechezwa kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, mechi za ushindi zikiwa ni 62 na 17 zikienda sare.

Jumla ya mabao 140 yameshafungwa mpaka sasa, wakati mechi 37 timu zimeshinda nyumbani, huku mechi 25 timu zikiwa zimeshinda ugenini.

## Bondia Kiduku atoa ahadi Moro

**Na Frank Kaundula, MOROGORO.**

BAADA ya kupata mapokezi makubwa kutoka kwa mamia ya wakazi wa Mkoa wa Morogoro waliojitokeza kumpokea wakati akitokea jijini Dar es Salaam kumtwanga Mthailand Sirimongkhon Jitbanjong kwa Technical Knockout (TKO), Bondia Twaha Kiduku ameahidi kuendelea kuilinda heshima hiyo kila apandapo ulingoni.

Wananchi waliojitojeza kumpokea bondia huyo walisema kujitokeza kwao kwa wingi kumetokana na Kiduku kuuleta heshima kubwa Mkoa wa Morogoro na taifa kwa ujumla kwa kupata ushindi huo.

Shabani Mahamudu akiwa miongoni mwa mashabiki wa bondia huyo waliojitokeza kumpokea, alisema Mkoa wa Morogoro umejaliwa kuwa na mabondia wengi na maarufu ukianza na Francis Cheka na Kiduku.

"Tumeamua kijitokeza kwa wingi kumpokea kijana wetu, kwani ametuletea heshima kubwa kama alivyokuwa akifanya Cheka, hivyo mapokezi haya ni kuonyesha wananchi wa mkoa huu tupo nyuma yake,"alisema Mahamudu.

Naye Hamisi Bakari, alisema: "Ili kijana huyu aendelee kufanya vizuri, anatakiwa kutobweteka na kulewa sifa kwa ushindi huo na badala yake endelee kujituma zaidi katika kufanya mazoezi kila mara."

Kwa upande wa Kiduku, alieleza kufurahishwa na mapokezi makubwa kutoka kwa wananchi wa mkoa wake ambapo aliahidi kuendelea kuilinda heshima hiyo waliyompa kila apandapo ulingoni.

## Judo wajifua kwa mashindano Z'bar

**Na Shufaa Lyimo**

UONGOZI wa Chama cha Mchezo wa Judo Tanzania (JATA), umesema tayari timu zote zinaendelea na mazoezi kwa ajili ya kujiandaa na mashindano ya Klabu Bingwa yatakayofanyika mwishoni mwa mwaka huu visiwani Zanzibar.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Katibu Mkuu wa chama hicho, Inocent Malya, alisema mashindano hayo yatakayoshirikisha klabu zote za Tanzania Bara na Visiwani lengo lake ni kupata timu nzuri ya taifa.

"Tunajiandaa na mashindano ya Klabu Bingwa kila timu inaendelea vizuri na mazoezi ," alisema Inocent.

Katibu huyo alisema katika mashindano hayo ambayo hufanyika kila mwaka, mshindi atakayepatikana atazawadiwa fedha taslimu kiasi kikitegemeana na mdhamini watakayempata.

Aidha, aliwataka Watanzania kujitokeza kwa wingi kujiunga na mchezo huo na kuacha dhana ya kuona ni mchezo wa hatari.

# Michezo

Jumanne Novemba 3, 2020

Nipashe




ARTETA ACHAMBUA REKODI ARSENAL...

HABARI UK 22




Kiungo wa Manchester United, Bruno Fernandes, akijaribu kumdhibiti kiungo wa Arsenal, Thomas Partey, kwenye mechi ya Ligi Kuu England iliyopigwa Uwanja wa Old Trafford juzi. Arsenal ilishinda kwa bao 1-0. **HABARI UK. 20**

# MO, HANS POPPE SASA WALIA HUJUMA SIMBA

## ●●●Waanika kila kitu, Bodi ya Ligi yashtuka yawataka kuwasilisha mezani, huku...

**Na Adam Fungamwango**

MJUMBE wa Bodi ya Wakurugenzi wa Klabu ya Simba, Zacharia Hans Poppe, amesema timu yao imekuwa ikihujumiwa na watu wa ndani na nje ya klabu hiyo, kiasi cha kusababisha kupoteza mechi mbili mfululizo za Ligi Kuu dhidi ya Tanzania Prisons na Ruvu Shooting.

Wakati Has Poppe akisema hayo, Mwekezaji wa klabu hiyo, Mohammed "Mo" Dewji naye ameibuka na kuandika kwenye mtandao wake wa kijamii akidai kuna hujuma zinazoendelea kwenye timu yao ya Simba.

Akizungumza jijini Dar es Salaam, Has Poppe alisema baadhi ya waamuzi pia wamekuwa moja ya wahujumu wa timu yao kutokana na uchezeshaji wao ambao unatia shaka kwa siku za hivi karibuni.

"Kuna hujuma imetembea, na sisi kama viongozi tumechukua hatua stahiki ikiwamo kuwaondoa baadhi ya watu. Ukiona mtu ameondolewa ndani ya klabu yetu, ujue amehusika kwa njia moja ama nyingine kwenye mpango huo wa hujuma dhidi ya timu," alisema Hans Poppe.

Akifafanua kauli yake, Mwenyekiti huyo wa zamani wa Kamati ya Usajili ya Simba, alisema hujuma zilianza kwenye mechi yao dhidi ya Prisons ambapo mbali na mwamuzi Shomari Lawi kutowapa penalti mbili za wazi, lakini pia aliachia wachezaji wa Prisons kufanya rafu mbaya za makusudi dhidi ya wachezaji wa Simba kiasi cha kuwafanya kuingiwa na woga wa kucheza mpira kwa kuhofia kuumia.

"Mwamuzi anatakiwa alinde wachezaji ndani ya uwanja, kuna rafu zingine mbaya zilikuwa zikichezwa ni za kadi nyekundu moja kwa moja, lakini hakutoa hata kadi ya njano," alisema kiongozi huyo.

Alisema wao kama viongozi wa Simba walikaa chini na kuanza kutafakari na kufanya uchunguzi na kubaini kuwa kuna mchezo mchafu unachezeka dhidi yao ili kuwadhoofisha.

"Kwenye mechi dhidi ya Ruvu Shooting napo tukagundua kitu kingine, kwa hiyo tukajua kuna hujuma kwa watu wa nje na wa ndani kwenye klabu yetu. Unajua klabu ya Simba jinsi ilivyosajili, haiwezekani ifungwe kirahisi na kwa namna ile kwenye mechi za ligi, kwa hiyo mara tulipofungwa ilibidi tutafute sababu na tukaipata," alisema Hans Poppe. Pamoja na kushinda mabao 5-0 dhidi ya Mwadui FC, alisema hata mechi hiyo iliyopigwa Jumamosi, kwa namna ya kushangaza walikataliwa mabao yao mawili ambayo kwa picha za marudio yalionekana kuwa ni sahihi.

"Hebu fikiria, kama Simba isingepata mabao mengine ingekuwaje? Si yangekuwa yale yale ya hujuma?" Alihoji Poppe.

Kwa upande wa Dewji, aliweka picha ya video ya moja ya bao lililokataliwa kwenye mechi kati ya timu hiyo dhidi ya Mwadui FC na kuandika ujumbe uliosomeka: "Bado dhuluma juu yetu inaendelea. Kwa mwenendo huu mpira wetu hapa Tanzania kamwe hauwezi kusonga mbele."

Hata hivyo, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Bodi ya Ligi nchini (TPLB), Almasi Kasongo, alisema hajaiona posti hiyo ya Mo, hivyo hawezi kusema au kujibu chochote, lakini amewataka wale wote ambao wana malalamiko au maoni kuyawasilisha rasmi kwao ili wayafanyie kazi, badala ya kuishia kuyasemea pembeni.

Simba ilipoteza mechi mbili mfululizo Oktoba 22, ilipochapwa bao 1-0 dhidi ya Prisons na Oktoba 26, ilipodunguliwa kwa kipigo kama hicho dhidi ya Ruvu Shooting na kuzusha mtafaruku mkubwa kutoka kwa wanachama na mashabiki wao, kiasi cha kusababisha kutimuliwa kwa Meneja wa timu, Patrick Rweyemamu, Kocha wa Makipa, Mwarami Mohamed na baadhi ya watendaji wengine.

# YANGA YAPANIA KUISHUSHA AZAM

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI Kocha Mkuu wa Gwambina FC, Novatus Fulgence, akieleza kwamba wamepania kuwa timu ya kwanza kuisimamisha Yanga katika mbio zao za kushinda mfululizo, wapinzani wao hao mkakati wao ni kuvuna pointi zote tisa wakiwa Kanda ya Ziwa, lakini wakilenga kuishusha Azam FC kileleni.

Gwambina iliyopo nafasi ya 14 kwenye msimamo wa Ligi Kuu Bara ikiwa na pointi tisa baada ya mechi tisa, itakuwa mwenyeji wa Yanga leo katika uwanja wao uliopo Misungwi nje ya Jiji la Mwanza katika mchezo utakaopigwa saa 10:00 alasiri.

Yanga iliyoshuka dimbani mara nane ipo nafasi ya pili ikiwa na alama 22 sawa na Azam FC iliyopo kileleni kutokana na tofauti kubwa ya mabao ya kufunga na kufungwa, lakini yenyewe ikishuka dimbani mara tisa.

Kocha wa Gwambina, Novatus alifunguka: "Nimesikia wanasema wamejipanga kuondoka na pointi tisa Kanda ya Ziwa, wamefanikiwa kupata sita, ila kwetu haitakuwa rahisi kama wanavyofikiria, pia haijawahi kutokea kuondoka na alama hizo hata wawe fiti kiasi gani."

Lakini Kocha Mkuu wa Yanga, Cedric Kaze, amesema mkakati wao ni kuhakikisha wanarejea na pointi tisa kutoka Kanda ya Ziwa baada ya kufanikiwa kuvuna sita kwa kuichapa KMC mabao 2-1 katika Uwanja wa CCM Kirumba na kisha kuibanjua Biashara United kwenye Dimba la Sokoine mjini Musoma.

"Bado timu yangu haijaanza kucheza kama ambavyo ninataka icheze, lakini cha muhimu kwanza ni kupata pointi tatu ambazo vijana wangu wamekuwa wakizipigania na hilo ndilo tunalolitaka kwa sasa," alisema.

Endapo Yanga itashinda mechi hiyo ya leo itafikisha pointi 25 na kuishusha Azam FC kileleni, huku timu hizo zikiwa zimecheza mechi tisa kila moja.

Kuelekea mechi hiyo, jana Ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli, aliliambia Nipashe kuwa timu yao ilitarajia kwenda kujifua katika Uwanja wa Gwambina, Misungwi ili kuzoea na kisha kurejea kambini jijini Mwanza walipoweka kambi na leo asubuhi ndipo watarejea tena Misungwi kwa ajili ya mchezo huo.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002